# Nipashe

Jumanne Februari 21, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581228

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US









**UFAFANUZI** dawa zilizoisha muda wake wa matumizi

UKURASA 2



Nipashe TESA

Mlango unaowainua wasichana kwenye sayansi unapofunguka

Makonda daladala kwa mateso haya wanazalisha kizazi hatari

UKURASA 11

# Vigogo wachunguzwa

## • Wadaiwa kuzipa tenda kampuni zao miradi, usambazaji vifaa... *Endelea uk. 2*



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa pili kushoto), Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Dk. Nkundwe Mwasaga (kushoto), Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, Dk. Amos Nungu (wa pili kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Mwambapa, wakionyesha mikataba ya makubaliano iliyotiwa saini na taasisi hizo kwa ajili ya utekelezaji wa programu ya IMBEJU iliyojikita kwenye uwezeshaji wa biashara bunifu za wanawake na vijana kiuchumi, Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

### ACT KUCHUNGUZA GHARAMA UKARABATI MV MAGOGONI

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kinafanya uchunguzi kuhusu gharama zitakazotumika kufanyia marekebisho ya kivuko cha MV Magogoni nje ya nchi zinazofikia Sh. bilioni 7.5...

UKURASA WA 4

### CRDB YAINGIA UBIA NA ICTC, COSTECH KUZIWEZESHA BIASHARA CHANGA

KATIKA mwendelezo wa kusaidia jitihada za serikali kukuza ujumuishi wa kiuchumi nchini, Benki ya CRDB imeingia mkataba wa makubaliano na Tume ya TEHAMA (ICTC) na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ...

UKURASA WA 5

### ATCL YAELEZA SABABU NDEGE MBILI KUSIMAMA

SHIRIKA la Ndege Tanzania (ATCL), limesema ndege zake mbili ndizo zimesimama kufanya kazi kutokana na hitilafu ya kiufundi lakini zingine nane zinaendelea kufanya ...

## Nabi ataja sababu tatu Yanga kuiua TP Mazembe

UKURASA. 24


# Wagonjwa uvimbe kwenye ubongo waongezeka MOI

UK. 2


MICHEZO SIMBA HASIRA CAF KWA AZAM FC LEO UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Vigogo TAMISEMI, TARURA wachunguzwa

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

SERIKALI imeanza kuchunguza na itatoa orodha ya baadhi ya watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, ikiwamo na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), wenye kampuni binafsi za ujenzi au uuzaji vifaa vya ofisi kwa kuwa wanasababisha kuwapo mgongano wa maslahi.

Aidha, mtumishi yeyote atakayebainika kwenye uchunguzi huo, hatua za kisheria zitachukuliwa kwa kuwa wanakwenda kinyume na maadili ya utumishi wa umma.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, aliyasema hayo jana jijini hapa katika mkutano wake na wahandisi na sekretarieti za mikoa, mameneja wa mikoa na wilaya wa TARURA na wakuu wa idara ya miundombinu na maendeleo ya vijijini na mijini kwenye mamlaka za serikali za mitaa.

"Kwa wale wenye kampuni ni vyema kutojihusisha na kazi kwenye taasisi zenu. Hata kama uko Wilaya X huruhusiwi kufanya kazi Wilaya Y. Atakayebainika hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

"Mtu hawezi kujichukulia hatua wala kujichunguza pindi inapotokea changamoto kwa kuwa itamletea mgogoro mkubwa. Serikali haiwezi kuvumilia hilo kwa kuwa kufanya hivyo ni kukiuka maadili ya utumishi wa umma.

Wale wenye kampuni binafsi ni vyema mkaepuka kujihusisha na utekelezaji wa kazi zilizoko katika taasisi zenu," alisema.

"Inawezekana ukawa unafikiri serikali haina macho, serikali macho inayo na tayari tunayo orodha ya baadhi ya waliofanya, hivyo tuwahakikishie kwamba tunao mkono mrefu wa kuwafikia," alisisitiza.

Aidha, alisisitiza watumishi hao kutimiza wajibu wao kwa ufanisi hasa kusimamia fedha zote zinazopelekwa katika halmashauri ili zitumike kwa wakati na kuzingatia thamani ya fedha.

Naibu Waziri wa TAMISEMI, David Silinde, alisema TARURA imekuwa ikifanya kazi nzuri na kutaka viongozi kutangaza utekelezaji wa miradi mkubwa inayofanyika ili wananchi wajue.

Awali, Mtendaji Mkuu wa TARURA, Mhandisi Victor Seff, alisema wakala unatekeleza mpango mkakati wa miaka mitano ambao umelenga kufikia asilimia 85 ya barabara ninazozihudumia zinapitika katika vipindi vyote vya mwaka na kuwa utekelezaji wake unatarajia kugharimu Sh. trilioni 4.2.

Alisema hadi sasa wamefanyia kazi ya ukarabati wa miundombinu ya mtandao wa barabara wenye kilometa 144,419 katika mikoa na halmashauri nchini.

Kwa mujibu wa Seff, mtandao wa barabara wenye urefu wa kilometa 38,868 zina hali nzuri, kilometa 48,307 zipo katika hali ya wastani na kilometa 57,000 zipo katika hali mbaya.



Mchuuzi wa mboga (kulia) akisaidiwa kutua mzigo na mteja wake katika kitongoji cha Kwa Mkolemba, Kipunguni Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Ufafanuzi dawa zilizoisha muda wake wa matumizi

**Na Mwadishi Wetu**

KATIKA gazeti hili tolea la Februari 18, mwaka huu, kulikuwa na habari yenye kichwa kilichosomeka 'Wagonjwa wapewa dawa zilizokwisha muda wa matumizi'.

Chanzo cha habari hiyo ni Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Shinyanga, Donasian Kessy, aliyekuwa akitoa taarifa ya utendaji wa taasisi katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2022.

Baada ya kusoma taarifa kwa umma iliyotolewa na Mkuu wa TAKUKURU Mkoa na sauti iliyorekodiwa na Mwandishi Wetu wakati kiongozi huyo akizungumza na vyombo vya habari, tumejiridhisha kwamba habari hiyo ilikuwa sahihi, isipokuwa kichwa cha habari kinakinzana na maudhui yaliyomo.

Kwa mantiki hiyo, tunaomba radhi juu ya mkanganyiko na usumbufu uliojitokeza kwa wahusika na jamii kwa ujumla kutokana na habari hiyo.

\- **MHARIRI**

# Wagonjwa uvimbe kwenye ubongo waongezeka MOI

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), imesema katika kipindi cha miaka mitano, imepokea wagonjwa 1,724 wenye tatizo la uvimbe kwenye ubongo.

Aidha, kwa mwaka wanapokea wagonjwa 340 na wagonjwa 25 hadi 30 kwa wiki wenye tatizo hilo.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Respicious Boniface, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika uzinduzi wa kongamano la kimataifa la madaktari bingwa wa ubongo ambalo limejikita katika matibabu ya uvimbe kwenye ubongo. Kongamano hilo la siku tano ni ushirikiano baina ya MOI na Chuo Kikuu cha Colorado nchini Marekani, ambalo limehusisha madaktari wanafunzi, walioko kazini na wakufunzi, litahusisha pia upasuaji kwa wagonjwa wenye uvimbe kwenye ubongo.

"Uwekezaji uliofanywa na Wizara ya Afya wa kununua vifaa vya uchunguzi, umesababisha kuongezeka kwa wagonjwa tofauti na miaka ya nyuma," alisema Dk. Boniface.

"Tupo hapa kufundishana mbinu mpya za kutibu. Udaktari ni sayansi, hivyo kila siku tunajifunza mbinu mpya na salama zaidi za kutibu haya magonjwa. Hili ni kongamano la pili na tumekutana madaktari bingwa wa Tanzania na nchi zingine. Tunaamini baada ya kongamano wataalamu watakuwa wameiva zaidi," alisema.

Dk. Boniface alisema hakuna sababu maalum za ugonjwa huo isipokuwa kwa watu wanaofanya kazi na kukaa karibu na migodini. Alitaja dalili za ugonjwa huo ni maumivu ya kichwa, kutapika, mwili kupooza na kuanguka kifafa.

Naye Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara ya Afya, Edward Mbaga, alisema jukumu la wizara hiyo ni kutengeneza mipango na sera na kuwapo kwa kongamano hilo ni utekelezaji wa sera ya mwaka 2017.

"Lengo ni kuhakikisha huduma za afya zinawafikia Watanzania na kupatikana kwa uwezo na umahiri mkubwa. Tukio la leo (jana) lina utekelezaji wa sera kwa sababu wenzetu wa MOI wakishirikiana na wenzao wa Marekani, wameandaa kongamano hili ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma za kibingwa hasa za magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama uvimbe kwenye ubongo," alisisitiza.

Mbaga alisema takwimu zinaonyesha wananchi wengi wanapata huduma za kibingwa nchini, kunakosaidia kupunguza safari za kwenda nje ya nchi kutibiwa ambako mgonjwa mmoja inamgharimu zaidi ya Sh. milioni 30.

Mkurugenzi wa Mradi wa Uvimbe Kwenye Ubongo kutoka Marekani, Ryan Ormond, alipongeza juhudi za serikali na ushirikiano waliopata kutoka MOI ili kubadilishana uzoefu katika utoaji wa huduma za kibingwa kwa madaktari wa nchi mbalimbali.




Wafanyakazi wa kujitolea kutoka Marekani wakiwa pamoja baada ya kuwasili Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: UBALOZI WA MAREKANI**

# ACT kuchunguza gharama ukarabati MV Magogoni

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kinafanya uchunguzi kuhusu gharama zitazotumika kufanyia marekebisho ya kivuko cha MV Magogoni nje ya nchi zinazofikia Sh. bilioni 7.5.

Kimedai gharama zilizotajwa na Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) kufanya ukarabati, zinaibua maswali yenye utata kutokana na bei ya ununuzi wa kivuko hicho kuwa Sh. bilioni nane.

Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, aliyesema hayo jana katika mahojiano na Kituo cha Redio cha Clouds FM jijini Dar es Salaam, akielezea masuala mbalimbali ya kijamii, kisiasa na kiuchumi na mapendekezo ya chama chao.

Alisema chama hicho kupitia Baraza Kivuli la Mawaziri kimemtaka Waziri Kivuli wa Uchukuzi kulifuatilia kwa kina suala hilo kwa kuwa 'gharama hizo zinafikirisha, zinatia hasira na suala hilo linapaswa kufikiriwa kwa kina na kuhojiwa.

"Juzi tulikuwa na kikao na Baraza Kivuli la Mawaziri. Wananchi wana haki ya kuhoji, huwezi ukatengeneza chombo kwa Sh. bilioni nane, ukarabati kwa Sh. bilioni 7.5.

"Tumemwagiza waziri wetu Mwalimu Macheyeki alifanyie kazi, tupate majawabu kabla ya kwenda huko au isiende kabisa," alisema Zitto.

Pia alidai kuwa mfumo wa uanzishwaji 'plea bargaining' haukuwa na tatizo, bali mchakato wake haukufuata sheria, hivyo waliohusika wanapaswa kushughulikiwa kisheria.

"Ni lazima kuwe na uwajibikaji kwa sababu usipofanya hivyo, atakapokuja mwingine atafanya hivyo. Kuna nchi ambazo zinafanya 'plea bargaining', ila tulipoanza sisi hatukuwa na sheria.

"Watu walianza kuingia makubaliano na serikali ya kutoa fedha, hakuna sheria. Lazima kuwe na sheria. Uwe na sheria kwanza halafu kanuni na utekelezaji vianze, lengo la 'plea bargaining' ni kurahisisha mfumo wa haki, kesi ziishe haraka, mtu akakiri kama alikosea, apigwe faini. "Ila dola, ofisi ya DPP na mahakama iligeuka kuwa kitengo cha mamlaka ya mapato. Nilichojifunza kutoka utawala wa awamu ya tano ni uwezo wa kuchukua uamuzi kwenye utendaji kazi, si katika kuamini uhuru wa kidemokrasia maeneo mbalimbali," alisema Zitto.

Akizungumzia bei za vyakula kupanda nchini, husussan nafaka, Zitto alisema kuna haja kuongeza uzalishaji na kilimo chenye tija na si kufungia mazao kuuzwa nje, kama ambavyo wengi wanapendekeza.

"Theluthi ya Pato la Taifa ni kilimo na theluthi mbili ya Watanzania tunategemea kilimo, tuachane na mawazo ya kuzuia uuzaji, sio jibu. Tuwe na chakula cha kutosha, ukanda wote unatutegemea.

"Tunahitaji (Tanzania) tani milioni sita za mahindi kwa mwaka, basi tulime tani milioni 12, tunayo ardhi ya kuitosha, tuna mito, tufanye kilimo cha umwagiliaji," alisema Zitto.

# AG aweka pingamizi kesi ya uraia pacha

**Na Kulwa Mzee**

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali amewasilisha mapingamizi matatu akiomba shauri la kupinga sheria inayozuia uraia pacha litupwe kwa madai viapo vya waombaji vina makosa.

Pia amedai kuwa masharti ya kifungu cha nne cha Sheria ya Utekelezaji Wajibu na Haki, katika kutafuta haki za kikatiba yamekiukwa.

Shauri hilo lilitakiwa kuanza kusikilizwa jana Mahakama Kuu Masjala Kuu ya Dar es Salaam mbele ya jopo la majaji watatu, Obadia Bwegoge, Hamidu Mwanga na Mwenyekiti wa jopo, Jaji Mustafa Ismail ambaye hakuwapo.

Upande wa Serikali umeweka mapingamizi hayo ukidai viapo vina matatizo, saihi hazikuwekwa, na waombaji wanadaiwa kukiuka masharti ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Utekelezaji Wajibu na Haki, katika kutafuta haki za kikatiba.

Shauri la Kikatiba la Uraia pacha namba 18 la mwaka 2022 lilifunguliwa na Watanzania sita wanaoishi na kufanya kazi nje ya nchi, Shaban Fundi, Patrick Nhigula, Restuta Kalemera, Nkole Muya, Emmanuel Emmanuel na Bashir Kassam dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

Watanzania katika shauri hilo wanapinga Sheria ya Uraia kwenye vifungu vinavyozuia uraia pacha, kifungu cha 7(1) na (2) (c ), (4)(a) (6) vya Sheria ya Uraia ambavyo wanadai vinakiuka haki zao zingine za kikatiba

Waombaji hao wanaiomba mahakama itamke kuwa vifungu hivyo ni batili vinakiuka haki zao za Kikatiba kwa kuwa vinawanyanya haki ya asili isiyonyang'anyika yaani uraia wa kuzaliwa.

Wakili wa waombaji, Peter Kibatala, alidai mahakamani kuwa wadaiwa wameshajibu madai yao kwa maandishi na pia wamewasilisha pingamizi la awali.

Akielezea mapingamizi hayo nje ya mahakama, Wakili Kibatala alidai wajibu maombi wanadai kuna kasoro za kisheria katika hati za viapo vya wadai.

Hoja nyingine ya pingamizi ni kwamba hati ya madai hazikutiwa saini na wadai pamoja na wakili wao na kwamba kesi hiyo inakiuka masharti ya lazima ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Utekelezaji Wajibu na Haki, katika kutafuta haki za Kikatiba.

"Mahakama imepanga kulisikiliza kwanza mapingamizi kabla ya kusikiliza shauri la msingi na imepanga kulisikiliza Mei 2, mwaka huu," alidai Kibatala.

Mjibu maombi katika shauri hilo AG anawakilishwa na Wakili wa Serikali, Ayub Sanga.

Waombaji ambao wako nje ya nchi hawakuwapo mahakamani badala yake waliwakilishwa na Liberatus Mwang'ombe aliyesafiri kutoka Washington DC nchini Marekani, akiungana na wadau wengine wa uraia pacha walioko nchini.

Katika viapo vyao, Watanzania hao wanadai ni Watanzania wa kuzaliwa waliondoka nchini na kwenda Marekani, Uingereza na Canada wanakoishi na kufanya kazi ambako pia walishapata uraia.

Wanadai wameathirika kwa kitendo cha kunyimwa haki mbalimbali katika nchi yao waliyozaliwa kwa kuzingatia kwamba walipata uraia wa nchi hizo.

"Sisi ni Watanzania kwa damu na kwamba tunatamani kuendelea kuwa Watanzania , lakini kwa vifungu hivyo vya Sheria ya Uraia tunanyimwa haki hiyo. Haki tunazozikosa nchini tulikozaliwa ni kutokuwa na haki ya kumiliki ardhi na kwamba tunapotembelea nchini tunaishia kuishi katika nyumba za ndugu au hotelini," walidai katika hati zao za viapo.

Wanataja haki zingine wanazozikosa kuwa ni pamoja na kutokuchagua viongozi wala kushiriki kugombea nafasi ya umma katika uchaguzi nchini.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Mtumba,**
**S.L.P. 2888,**
**40470DODOMA,**
**21.02.2023**

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumatano tarehe 22-02-2023 kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Kilombero kupitia Mikumi,** gari hiyo ina namba ya usajili:

**T 167 DFC /T 568 EAZ**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 23.00, Upana - mita 4.30, Kimo - mita 4.80**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi,** gari itasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Mtumba,**
**S.L.P. 2888,**
**40470DODOMA,**
**21.02.2023**

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumatano tarehe 22-02-2023 kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Kilombero kupitia Mikumi,** gari hiyo ina namba ya usajili:

**T 419 DFE / T 499 DZX**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 23.00, Upana - mita 4.30, Kimo - mita 4.80**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi,** gari itasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

# Waziri Mchengerwa atangaza hatua maofisa wanaohujumu maliasili

Na Elizabeth Zaya

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, amesema atawachukulia hatua kali baadhi ya maofisa wanaoshiriki biashara ya uvunaji haramu misitu hifadhini katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro.

Akizungumza jijini Dar es Salaam wakati akikabidhi pikipiki zaidi ya 40 za kwenda kwenye mikoa mbalimbali kwa ajili ya kusaidia kuimarisha ulinzi na udhibiti kwenye maeneo ya uhifadhi, alisema zipo taarifa kwamba baadhi ya maofisa kushiriki uvunaji haramu wa raslimali hizo.

"Najua wako baadhi ya maofisa wetu wamekuwa wakishiriki katika biashara ambazo sio nzuri, ikiwamo uvunaji haramu, tunayo maelekezo ya moja kwa moja ya Makamu wa Rais, kuhusu tatizo kubwa la uvunaji katika mikoa ya Pwani na Dar es Salaam. Kwa hiyo nikuombe Mtendaji Mkuu TFS, hawa maofisa wanaohusika na mikoa hiyo katika maeneo ya hifadhi, wajitafakari,"alisema.

"Tunakwenda kubadilisha mifumo yote ya utendaji wa kimazoea ili kuhakikisha kile kinachokusudiwa na viongozi wetu kinatekelezwa. Kama walikuwa na tabia ya kuzembea, tutawapa muda wa kubadilika, kama hawaziwezi nafasi walizopewa watuambie tuwape wengine wenye uwezo wa kuzifanya.

Kwa mujibu wa Mchengerwa, atabadili mfumo wa utendaji na kuomba wale wote wanaozembea kujitafakari kama wanaweza nafasi hizo au wapishe wapewe wengine.

"Nikuombe Mtendaji Mkuu wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, hakikisha kwamba maofisa wanaohusika katika mikoa hiyo ya Pwani, Morogoro na Dar es Salaam, katika maeneo ya hifadhi wajitafakari kwa kuwa nakwenda kubadilisha mifumo yote ya utendaji," alisema.

Alisema kila mtendaji atateuliwa kwenye nafasi kwa kupimwa utendaji wake na si kwa bahati.

"Kila mtendaji atapimwa kwa namna anavyoweza utendaji wake wa kazi na kila atakayeteuliwa kwenye nafasi yake hasa watendaji kwenye mikoa na wilaya, nitawapima kwa utendaji wao.

"Hakutakuwa na vitu kutokea kwa bahati, kila atakayeteuliwa atakuwa ni yule ambaye ameaminiwa kwamba atafanya kazi ya udhibiti hasa uvunaji haramu ambao umezuiliwa, mahusiano baina yetu na wananchi," alisema.

Aliwataka watendaji kuacha kukaa ofisini na kwenda kusikiliza na kutengeneza uhusiano mzuri na wananchi.

"Kama kuna sehemu ambako tulikuwa tunatereza tukawa hatuko karibu na wananchi, inabidi sasa twende kwao na tukawape elimu, inawezekana wapo ambao walikuwa wanavuna pasipo taratibu huenda wengine taratibu hawazijui, tuwape elimu. Pia inawezekana tukabadilisha maisha ya wale wanoishi kwenye maeneo ya hifadhi."

Mchengerwa alisisitiza mambo matatu katika wizara hiyo ikiwamo utendaji kazi wa juhudi, ushirikiano na wa maadili.

Aliitaka TFS kuongeza udhibiti wa usimamizi ili iendelee kufanya vizuri zaidi kwenye uvunaji.

"Pamoja na kwamba TFS inafanya vizuri zaidi kwenye uvunaji, lakini ninaamini kwamba mkiongeza nguvu zaidi katika udhibiti kwenye hifadhi zetu za misitu mtavuna zaidi."

Naye Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Prof. Dos Santos Silayo, alisema zaidi ya pikipiki 40 walizokabidhi katika mikoa mbalimbali zitasaidia kazi ya udhibiti kwenye hifadhi mbalimbali za misitu na maeneo mengine ambayo wakala huyo anafanya kazi. Alisema TFS inapaswa kuwa na vifaa mbalimbali vya kusaidia utekelezaji wa shughuli zake kwa ufanisi zaidi ikiwamo vifaa vya zimamoto, magari na kwamba tayari baadhi wanavyo ikiwamo boti kwa ajili ya shughuli zao.

Prof. Silayo alisema tangu wameachana na utendaji kazi wa kiraia na kwenda kwenye utendaji wa kijeshi vifaa hivyo ni muhimu sana katika utekelezaji wa shughuli zao kwa ufanisi..




Wakili Peter Kibatala (wa pili kulia) na wanajumuiya ya Watanzania waishio nje ya nchi - diaspora wakitoka kwenye Mahakama Kuu ya Tanzania baada ya kuahirishwa kwa shauri la kikatiba la uraia pacha jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# CRDB yaingia ubia na ICTC, COSTECH kuziwezesha biashara changa nchini

Na Mwandishi Wetu

KATIKA mwendelezo wa kusaidia jitihada za serikali kukuza ujumuishi wa kiuchumi nchini, Benki ya CRDB imeingia mkataba wa

makubaliano na Tume ya TEHAMA (ICTC) na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kupitia programu yake ya 'IMBEJU' iliyojikita katika uwezeshaji wa wanawake na vijana kiuchumi.

Akizungumza katika hafla ya kutia saini mkataba wa makubaliano, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela alisema jijini Dar es Salaam jana kuwa ushirikiano na taasisi hizo za serikali utasaidia kufanikisha malengo ya programu kwa kiasi kikubwa kutokana na jinsi uzoefu

wa taasisi hizo katika kuwawezesha vijana wabunifu kwenye sekta mbalimbali.

"Ili kuifanya programu hii kuwa yenye ufanisi na kufikia walengwa wengi, tumeona ni vyema kutafuta wadau ambao wana mawazo kama yetu yaani 'like-minded partners'.

ICTC na COSTECH wamekuwa wakifanya kazi nzuri ambayo inaakisi utayari wa serikali yetu katika kukuza biashara na mawazo ya ubunifu, hivyo tunajivunia kwa hatua hii muhimu," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya TEHAMA, Dk. Nkundwe Mwasaga, alisema mkataba wa makubaliano walioingia na Benki ya CRDB utakwenda kusaidia upatikanaji wa mitaji wezeshi kwa biashara changa katika sekta ya TEHAMA pamoja na kutoa usaidizi wa kuboresha mawazo na biashara bunifu, jambo litakalosaidia kukuza ajira nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa COSTECH, Dk. Amos Nungu, alisema makubaliano waliyoingia na Benki ya CRDB yanakwenda kuoanisha IMBEJU na programu za taasisi hiyo zinazochochea ubunifu wa kibiashara ikiwamo MAKISATU, jambo litakalosaidia kuchochea kasi ya ukuaji wa biashara changa katika sekta mbalimbali.

Katika hafla hiyo, Benki ya CRDB pia iliutangazia umma kuanzishwa kwa taasisi isiyo ya faida ya 'CRDB Bank Foundation' yenye jukumu la kuanzisha na kutekeleza programu bunifu, endelevu na shirikishi zinazolenga kuleta ustawi wa kijamii na kiuchumi kama IMBEJU.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Nsekela, alimtambulisha Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB, Tully Esther Mwambapa, kama Mkurugenzi Mtendaji Mwanzilishi wa taasisi hiyo ya CRDB Bank Foundation.

Akizungumza kwa mara ya kwanza kama Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully aliwataka vijana wabunifu kuchangamkia fursa inayotolewa na benki hiyo kupitia programu ya IMBEJU inayotekelezwa kwa kushirikiana na ICTC na COSTECH.

"Mkataba tulioingia leo (jana) unatupa uwezo wa kushirikiana na ICTC na COSTECH kufanya utambuzi wa biashara changa bunifu zinazohitaji usaidizi. Niwaombe vijana kutumia mifumo ya utambuzi ya taasisi hizi ili kunufaika na fursa hii," alibainisha Tully.

Pia alitumia fursa hiyo kuwaalika vijana kushiriki semina maalum ya uwezeshaji iliyoandaliwa na Benki ya CRDB, ikipangwa kufanyika Machi 11, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC), ambapo programu hiyo itaingizwa sokoni rasmi na uwezeshaji kuanza kufanyika.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

# Rufani kesi ya Sabaya yakwama kusikilizwa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha imeshindwa kuendelea na usikilizaji wa rufani ya kesi ya uhujumu uchumi namba 27 iliyokuwa inamkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake watano baada ya wajibu rufani kwenda Mahakama ya Rufani kuomba ifanye mapitio ya mwenendo wa shauri hilo pamoja na uamuzi mdogo uliotolewa Desemba 14, mwaka jana.

Katika rufani hiyo namba 155/2022, waleta rufani ni Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na wajibu rufani ni Ole Sabaya, Silvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Desemba 13, 2022 mawakili wa wajibu rufani waliwasilisha mahakamani hoja mbili za kupinga kusikilizwa kwa rufani hiyo, wakidai kuwa rufani hiyo haikuwa sawa kisheria.

Pia walikuwa na hoja kwamba DPP aliweka kusudio la kukata rufani kwa waliokuwa washtakiwa saba, lakini rufani iliyowasilishwa mahakamani, ilionyesha waliokatiwa rufani ni watu sita badala ya saba.

Desemba 14, mwaka 2022, Jaji wa Mahakama hiyo, Salma Maghimbi, akitoa uamuzi mdogo alisema kuwa baada ya kupitia mawasilisho ya hoja za pande zote mbili, mahakama imejiridhisha kuwa rufani iliwasilishwa ndani ya muda husika.

Jana mahakamani huko, Wakili wa Serikali Mwandamizi Filex Kwetukia alidai kuwa shauri hilo lilipangwa kwa ajili ya kwenda kusikilizwa lakini Februari 3, mwaka huu, walipokea notisi kutoka Mahakama ya Rufani kuwa imeombwa na wajibu rufani kufanya mapitio ya mwenendo pamoja na uamuzi mdogo wa Mahakama Kuu Masjala ya Arusha uliotolewa Desemba 14, 2022 katika kesi hiyo.

Alidai kwa msingi huo, kwa kuwa kuna maombi ya mapitio ya mwenendo wa kesi hiyo na uamuzi mdogo, ni rai yao kwamba rufani hiyo isubirie kwanza uamuzi utakaotolewa na Mahakama ya Rufani.

"Shauri lilikuwa limepangwa kusikilizwa lakini Februari 3, 2023 tulipokea notisi kutoka Mahakama ya Rufani ya kuomba kufanya mapitio ya mwenendo wa kesi pamoja na uamuzi uliotolewa Desemba mwaka jana," alidai Wakili Kwetukia.

Wakili wa Wajibu Rufani katika shauri hilo, Mosses Mahuna, alidai kuwa upande wao hauna pingamizi na maelezo yaliyotolewa na Wakili wa Jamhuri.

Jaji Maghimbi alisema kuwa kutokana na maombi ya wajibu rufani hao kwa Mahakama ya Rufani, shauri hilo litasimama kwa muda hadi hapo uamuzi utakapotolewa.

Katika shauri hilo, shtaka la kwanza ni la kuongoza genge la uhalifu kinyume cha Sheria ya Uhujumu Uchumi kifungu cha 57(1) na 60(2), lilikuwa linawakabili washtakiwa wote.

Shtaka la pili ni kujihusisha na vitendo vya rushwa na lilikuwa linamkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake na shtaka la tatu ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa lililomkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake.

Shtaka la nne ni matumizi mabaya ya madaraka lililomkabili Sabaya peke yake na la tano ni utakatishaji wa fedha, lililowakabili washtakiwa wote.

# ATCL yaeleza sababu ndege mbili kusimama

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Ndege Tanzania (ATCL), limesema ndege zake mbili ndizo zimesimama kufanya kazi kutokana na hitilafu ya kiufundi lakini zingine nane zinaendelea kufanya safari kama kawaida.

Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Ladislaus Matindi, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ujio wa ndege mpya ya mizigo na maendeleo ya shirika hilo.

"Ndege zetu ziko 11 mpya zilizonunuliwa na serikali lakini ya 12 tuliirithi na ilikuwa na umri kidogo na tangu 2017 haijafanyakazi iko matengenezo kwa sababu ilihitaji matengenezo makubwa," alisema Matindi.

Alisema kati ya ndege hizo, mbili zinafanya safari za masafa marefu, nne za masafa ya kati aina ya Airbus 220 (300), tano za masafa mafupi aina ya DASH 8 Q(400) Bombardier zinatumika kwa safari za ndani na za karibu ya nchi.

"Kwa hiyo ndege zetu ambazo hazifanyi kazi ni tatu tu. Mbili zina tatizo la injini ambalo ni la kawaida hata kwa kampuni za wenzetu kama Egypt Air na Swiss Air wana shida kama hiyo na ndege moja ina tatizo la kisheria ambalo Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) ndiye anaweza kulielezea vizuri sana," alisema.

Matindi alisema ndege kubwa aina ya Boeing 787 Dreamliner za ATCL zinafanya safari za nje na zimetengenezwa kwa ajili ya kufanya safari ndefu.

"Tulikuwa tunafanya safari India mara tatu kwa wiki lakini tulikuwa tunaenda China mara moja kwa wiki kwa sababu sisi tulitaka twende mara tatu ila wao wakatupa nafasi moja.

"Tumeomba na tumeruhusiwa sasa tutakwenda China mara mbili kwa wiki. Tulipitia kipindi kigumu cha UVIKO -19 na China walikuwa na masharti magumu sana lakini sasa wameyaondoa," alisema.

Matindi alisema bei zilipanda sana lakini kuanzia Machi 2, mwaka huu, wanaongeza safari nyingine ya kila Alhamisi na kwamba hiyo imetokana na mahitaji ya soko.

"Nauli kwenda China ni dola 1,060 lakini wakati ule nauli wa COVID - 19 ilifika hadi dola 4,000 na ilileta malalamiko lakini wafanyabiashara waelewe kwamba bei hazisababishwi na sisi, ilikuwa tatizo la soko kwa dunia nzima," alisema.

Alisema habari nzuri sasa ni kwamba wameongeza safari ya pili kwenda China na bei imeshuka kutokana na masharti yaliyowekwa na China kuondolewa.

"Tunawakaribisha Watanzania kutumia huduma za ATCL kwenda China mara mbili kwa wiki kuanzia Machi 2 ni safari ya saa 12 kwenda na saa 12 kurudi mara mbili kwa wiki na nauli ambayo inamvuto kwa wengi," alisema.

Pamoja na abiria, alisema shirika hilo linabeba mizigo kwenda China na mizigo kutoka China na aliwaomba wafanyabiashara kutumia shirika hilo kusafirisha mizigo yao.

Alisema ATCL ilikuwa na safari tatu kwa wiki kwenda India lakini kwa sasa zimeongezeka na kufikia nne na zinafanyika kila Jumatatu, Jumatano, Ijumaa na Jumapili.

"Kwa ndege zetu kubwa zitakuwa zinafanya safari mara sita kwa wiki tunaendelea kupanua soko letu na tunaangalia uhitaji wa abiria," alisema.

Kuhusu ujio wa ndege mpya, alisema kuna ndege nne ambazo ziko katika hatua za mwisho na ndege moja ya kwanza wanayotarajia kuipokea ni 767 ya mizigo ambayo itawasili mwezi Machi mwishoni.

Alisema serikali imeamua kununua ndege hiyo baada ya kubaini kuwapo kwa mahitaji makubwa ya ndege ya mizigo.

"Tunatarajia kama hakutakuwa na mabadiliko ndege hiyo itakuja mwezi wa tatu na mwezi wa nne itaanza kutoa huduma za mizigo kwenda na kurudi nje ya nchi na tunaendelea kuzungumza na wasafirishaji na watoa huduma ambao wamefurahia ujio wa ndege hiyo," alisema.

"Pamoja na hayo tuna ndege mbili za masafa ya kati tunaposema masafa ya juu ni zile ndege kubwa kabisa zinazoruka saa sita na kuendelea lakini kuna za masafa ya kati ambazo ni chini ya hizo saa aina ya 737 (Max 9) hizi ni ndege mbili kila mmoja inauwezo wa kubeba abiria 181," alisema Matindi.

Alisema ndege mbili zinatarajia kuwasili nchini mwezi wa nane na nyingine itawasili mwishoni mwa mwaka huu hali ambayo italiongezea uwezo shirika hilo.

Alisema pia shirika linatarajia kupokea ndege kubwa aina ya 787 Dreamliner yenye uwezo wa kubeba abiria 262 na kwamba nia ya shirika ni kuingia kwenye soko la Ulaya ifikapo mwaka 2024.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA KUWASILISHA NIA KWA AJILI YA KUSANIFU NA KUTEKELEZA PROGRAMU YA KUFANYA UTAFITI NA KUREJESHA MSITU WA MIKOKO NA ONGEZEKO YAKINIFU LA BIOANUAI YAKE KATIKA BAHARI YA MKOA WA TANGA KATIKA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) KUMB NA – REQ-00000157**

Kampuni ya EACOP inazialika kampuni zenye uzoefu na sifa kuwasilisha maombi ya nia ya kutoa huduma ya kuandaa, kusimamia na kutekeleza **"Kusanifu na Kutekeleza Programu ya Kufanya Utafiti na Kurejesha Msitu wa Mikoko na ongezeko yakinifu la bioanuai yake katika Bahari ya Mkoa wa Tanga"** katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP). Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litalofukiwa ardhini, linalokatisha mipaka ya nchi mbili ili kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi Pwani ya Mashariki mwa Tanzania kwa ajili ya Kwenda katika Masoko ya Kimataifa. Bomba litaanzia eneo la Kabaale Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, hadi eneo la Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA MAWANDA YA HUDUMA**

Kituo cha baharini cha Mradi wa EACOP cha Rasi ya Chongoleani kitakuwa na Sehemu iliyo nchikavu ya kuhifadhia mafuta, bandari (njia ya juu ya maji) yenye urefu wa kilomita 2 kuelekea ndani ya bahari, na sehemu ya kupakilia mafuta mwisho wa bandari (njia) hiyo. Katika ujenzi wa njia (bandari) hiyo na matumizi yake sehemu ndogo ya habitati ya Msitu wa Mikoko itaweza kuathiriwa. Mpango wa Utekelezaji wa Bioanuwai (Biodiversity Action Plan) umeshaandaliwa na umeonesha kiwango cha awali cha maeneo yatakayoweza kuathirika. Vifo vya mikoko magondi au mikoko myekundu (Rhizophora mucronate) vimetokea na kuandikwa mwaka 2021 na havihusiani kabisa na shughuli za EACOP.

Inahitajika Kampuni/Taasisi ya kufanya usanifu na utekelezaji wa programu ya urejeshaji wa habitati ya msitu wa mikoko; na kutafiti juu ya sababu zilizopelekea kufa kwa mikoko myekundu katika mdomo wa Mto Zigi, na matokeo ya utafiti huo yatumike katika utekelezaji wa urejeshaji wa mikoko katika Ghuba ya Tanga na kaskazini mwa Tanzania kwa ujumla ikilenga ongezeko halisi (Net Gains) na ikizingatia vigezo na mbinu bora. Njia ya kuyafikia hayo inatakiwa iwe shirikishi ambapo hatua zote zitajumuisha wadau wa ndani na vikundi vyengine, ikiwa ni pamoja na jumuiya za mitaa, taasisi za serikali na mashirika ya kiraia. Maamuzi ya kutekeleza njia au mbinu zitakazokubaliwa yanapaswa kuzingatia takwimu za kisayansi na kuhakikisha ubora wa maamuzi hayo kulingana na hali ya kijamii na mazingira yaliyopo hivi sasa na mwelekeo wa baadae.

**VIGEZO MUHIMU**

Kampuni zinazowasilisha nia zinapaswa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili kama shirika/taasisi ambayo shughuli zake zinahusiana na shughuli za ushirikishaji jamii (kwa mfano urejeshaji wa habitati za baharini unaoshirikisha jamii).
- Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa kupanga, kusanifu na kutekeleza programu za uendelezaji wa urejeshaji wa misitu ya mikoko, utafiti wa kufa kwa mikoko, kuanzisha vitalu vya miche ya mikoko, kufanya kazi kwa kushirikiana na kujenga uwezo wa jamii za pwani, kufanya utafiti, ufuatiliaji na utengenezaji wa ramani za mtandao wa misitu ya mikoko.
- Mifano ya kazi zinazoonyesha uzoefu wa kufanya kazi zinazofanana na hizo zilizofanywa kipindi cha karibuni, ndani miaka mitano iliyopitaLeseni ya biashara.
- Wasifu wa watendaji watakaohusika katika Mradi ikiwa ni Pamoja na nakala za vyeti vyao, kiwango cha elimu, uzoefu na uwezo wa kutoa huduma inayohitajika.
- Leseni inayofaa kutoka kwa mamlaka husika ya ndani ya nchi kwa ajili ya utoaji wa huduma hii
- Uthibitisho wa Usajili toka Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Cheti cha Uthibitisho wa Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni.
- Usajili katika Kanzi Data ya Watoa Huduma wa Ndani ya EWURA (LSSP) au ushahidi thabiti wa maombi ya usajili wakati wa uwasilishaji wa maombi ya nia hii iliyotangazwa.
- Kufuata/kukubaliana na kanuni za Wazawa za Mambo ya Petroli za Tanzania.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni Pamoja na kuwakilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita.
- Uthibitisho kutoka mfumo wa usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na viwango vya ndani na vya ki-sekta vinayotumika kwa kazi hii.
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za Haki za Binadamu, na kupinga rushwa na ufisadi.

Kampuni zenye nia uwezo na rasilimali ya kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinatakiwa kutuma maombi ya nia yaliyoandaliwa kwa lugha ya Kiingereza pamoja na nyaraka zilizobainishwa hapo juu kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop.com (ukubwa usiozidi MB20) kabla au si zaidi ya saa 11:00 jioni Majira ya Afrika Mashariki, tarehe 2nd March 2023.** Kichwa cha cha barua pepe kiwe: [REQ-00000157] _ 'Kusanifu na Kutekeleza Programu ya Kufanya Utafiti na Kurejesha Msitu wa Mikoko na ongezeko yakinifu la bioanuai yake katika Bahari ya Mkoa wa Tanga katika Mradi wa EACOP.

Maombi yote ya kuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.

Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.

**Muhimu:** EACOP itapitia na kuchambua nyaraka ziizotumwa na makampuni yalioonesha nia kulingana na EOI hii, na kisha kufanya tathmini kulighana na vigezo vya ndani vya EACOP ili kubaini makampuni yenye sifa yatakayojumuishwa kwenye orodha ya awali ya makampuni yenye vigezo. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD ina haki ya kuteua au kukataa kampuni na kubaki na maamuzi yake bila kutoa sababu kwa kampuni husika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Serikali ifanye ufuatiliaji utumikishaji wa wanafunzi*

**GAZETI** hili katika toleo la jana, lilichapishwa habari inayoeleza kazi nyumbani kwa mwalimu zilivyo kichaka cha ukatili kwa wanafunzi. Habari hiyo ni simulizi ya mtoto wa miaka 14 aliyekuwa mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Kazana Upate, Kata ya Igagala, Kaliua mkoani Tabora kupata mimba.

Mwanafunzi huyo alidai alibakwa na mwalimu na kupata ujauzito baada ya kuambiwa aende akamsaidie kuosha vyombo na alipohoji wenzake atakaokwenda kufanya nao hiyo kazi, alijibiwa atawakuta nyumbani kwa mwalimu.

Tukio hilo lilitokea mwaka 2020 baada ya binti huyo kwenda kwa mwalimu na dakika chache baadaye mwalimu huyo alifika. Alipomuuliza wenzake wa kusaidiana naye waliko, alimjibu wako ndani lakini alipofungua mlango na kuingia, mwalimu alifunga na kisha kumbaka.

Kwa mujibu wa mwanafunzi huyo, mwalimu huyo alimpa Sh. 1,500 akanunue dawa za maumivu na kumtishia kuwa atamwachisha shule iwapo atatoa siri hiyo na kumpa adhabu mara kwa mara, jambo ambalo lilimuumiza kimwili na kisaikolojia.

Mwalimu huyo, mwanafunzi anasema, alikuwa na mke ambaye ni dada wa mwanafunzi huyo wenye uhusiano kwa mama zao mkubwa na mdogo na kwamba wanafunzi tofauti huenda kwa mwalimu huyo na wengine kuwasaidia kazi za nyumbani kama kuteka maji na usafi wa nyumbani.

Baada ya kutendewa kitendo hicho, mwanafunzi huyo anasimulia kwamba muda mfupi aligundua amepata ujauzito na kuwa mwisho wa safari yake kimasomo na sasa analea mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka miwili.

Huyu ni mmoja kati ya wengi wanaokutana na mazingira kama haya na kufanyiwa ukatili. Wachache wanaweza kueleza walichotendewa lakini wengi wameishia kunyamaza bila kuchukua hatau zozote ili kuficha aibu inayoweza kuwapata.

Waliosoma maeneo ya vijijini wataafiki kuwa katika baadhi ya shule, walimu huwatumia wanafunzi kuwafanyia kazi za nyumbani. Wanafunzi hukubali kwa sababu walimu wao wamewataka kufanya hivyo wanafunzi walikuwa wanaona sawa lakini hivi sasa kunapokuwapo ukatili ndipo yanazua malalamiko.

Licha ya kuwapo kwa taratibu za uendeshaji shule na za nchi zinazotaka wanafunzi kutumia muda wao mwingi kwenye masomo, wanafunzi hasa maeneo ya vijijini, wamejikuta wakitumikishwa na walimu. Baadhi ya walimu hufanya hivyo kwa nia njema kwa kuwa wanafunzi wengine wanatoka kwenye familia duni zisizoweza kulipia chakula cha mchana, wengi wamejikuta kwenye mikono mibaya kwa kufanyiwa ukatili kama alivyosimulia binti huyo wa miaka 14. Kwa hali ilivyo sasa ni muhimu kamati za shule zikafuatilia kwa karibu sana maendeleo ya shule ikiwamo namna walimu wanawatumikisha wanafunzi na kukomesha vitendo hivyo, vinavyotoa mwanya kwa ukatili kufanyika.


Kwa sasa matukio ya ukatili dhidi ya watoto yameongezeka na kila wiki linaripitiwa tukio la ubakaji, ulawiti na ukatili mwingine jambo ambalo si sawa kwa ustawi wa watoto.

Ni imani kwamba kama kutakuwa na ufuatiliaji wa karibu, wanafunzi wataachwa kubaki kuwa wanafunzi na kufanya kazi za msingi za usafi na bustani za kujifunza kama ilivyo kwenye shule za umma.

Bila ufuatiliaji wa karibu wa kamati za shule na waratibu elimu wa kata, wanafunzi wataendelea kutumikishwa kwa mazingira yanayosababisha ukatili ambao unakatisha ndoto zao.

Ni vyema serikali ikaelekeza kamati za shule na wataribu elimu kuwa na utaratibu wa kuzungumza au kuweka utaratibu wa siri wa wanafunzi kueleza wanavyotumikishwa na kama kuna ukatili wanakutana nao kwenye nyumba za walimu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# *Ni uamuzi mgumu ila yapo manufaa*

**SERIKALI** imesisitiza kuendelea kufanya uchunguzi na kuchukua hatua na ikibidi inaweza kuzifuta shule nne zinazotuhumiwa kufanya udanganyifu, katika mtihani wa kidato cha nne uliofanyika mwaka jana.

Hatua hiyo ninaweza kuichukulia kama maamuzi magumu, lakini yenye manufaa katika elimu, kwani inaweza kuwafanya wale ambao wamekuwa wakijihusisha na vitendo hivyo vya udanganyifu kuogopa.

Wakiogopa wanafunzi kufaulu kulingana na uwezo wao wa darasani na sio ufaulu wa 'kupikwa' ambao kimsingi hauwezi kuwasaidia katika safari yao ndefu ya kielimu na kimaisha.

Maelezo ya Waziri wa Elimu, Profesa Adolf Mkenda, kuwa serikali itaendelea kufanya uchunguzi na kuchukua hatua, yangefaa kuwashtua wote wenye nia ya kuandaa mikakati ya kudanyanga ili wabadilike.

Tayari shule nne za Twiboke, Thaqafa, Cornelius Nemonic Academy na Paqfa matokeo yake ya kidato cha nne yamezuiwa, huku zikiendelea kuwa chini ya uangalizi.

Zaidi ya hapo, kwa mujibu wa waziri lolote linaweza kutokea akiwamo kuzifuta. Sasa linapokuja suala kama hilo, ninadhani ni vyema shule nyingine ambazo zimewahi kuguswa na tuhuma hizo kukaa mguu sawa.

Waswahili husema "ukiona mwenzio ananyolewa, na wewe tia maji". Shule hizo nne zinaendelea kung'ang'aniwa, hivyo ni vyema nyingi kuchukua hatua za kujirekebisha ili zisikutane na rungu la serikali.

Ninadhani njia nzuri ya kuzisaidia shule zenye mchezo huo, ni kujikita zaidi katika kuwaandaa vizuri wanafunzi, ili wafaulu kulingana na uwezo wao darasani, hatimaye waje kuwa manufaa kwa taifa lao.

Lakini kutegemea mbinu chafu ili kupata ufulu mkubwa, inakuwa ni sawa na kushawishi wazazi na walezi, wavutike na kupeleka watoto wao katika shule hizo wakiamini zinafundisha vizuri na kumbe sivyo.

Hatua iliochukuliwa na serikali na kukomaa na shule zinazotuhumiwa kufanya udanganyifu, ninadhani inaweza ikazifanya shule nyingine kubadilika na kuachana na mtindo wa muda mrefu wa kila mwaka kuwa na udanganyifu.

Uamuzi wa sasa wa wizara unaweza kuwa ni mwarobaini wa kukomesha mchezo huo, kwani kila mwaka NECTA hutoa onyo mapema kabla mtihani ikielekeza kutojihusisha na udanganyifu.

Lakini matokeo yanapotangazwa, huwa kuna taarifa za baadhi ya wanafunzi kufutiwa matokeo kutokana na udanganyifu. Kwa kuwa hiyo hujirudia kila mwaka, ninadhani uamuzi wa sasa wizara unaweza kuwa suluhisho.

Baadhi ya wanafunzi na wazazi watakuwa wameumia kutokana na hatua zilizochukuliwa na wizara, za kuzuia matokeo ya mtihani, lakini ninaamini lengo ni zuri la kuokoa elimu ya Tanzania.

Wakati mwingine, inawezekana kukawa na sababu nyingi zinazochangia kuwapo kwa mchezo huo, ikiwa baadhi ya walimu kutaka kujipatia kipato kwa njia hiyo, kutokana na ugumu wa maisha.

Kama hilo lina ukweli wake, ninadhani si sahihi kuhalalisha uovu huo, eti kwa sababu ya ugumu wa maisha, bali ni muhimu wawe mstari wa mbele kukemea vitendo hivyo ambavyo vinashusha kiwango cha elimu. Ninajua kwa sasa kuna ushindani katika elimu, lakini usiwe chanzo cha kufanya udanganyifu, bali nguvu kubwa ielekezwe kwenye ufundishaji, ili wanafunzi wafaulu kulingana na uwezo wao

wanafunzi wanasoma wakiwa na malengo ya kufaulu, wasonge mbele kielimu, hivyo ninadhani si vizuri kuwaacha wabweteke ili baadaye wafaulu kupitia udanganyifu. Hapo ni sawa kama hawajatendewa haki.

Ninadhani ufuatiliaji wa serikali katika matokeo ya mitihani umekuja kuibua mambo mengi yaliyokuwa yamejificha. Hivyo, ingefaa wahusika kuweka mkazo kwenye ufundishaji, ili wanafunzi wafaulu kwa akili zao.

## Muswada Sheria ya Habari kuchambuliwa kwa Kiswahili

**Na Mwandishi Wetu**

MUSWADA unaolenga kufanya mabadiliko ya Sheria ya Huduma za Habari 2016 uliowasilishwa bungeni Februari 10 mwaka huu, utachambuliwa kwa lugha ya Kiswahili ili ueleweke zaidi kwa wananchi.

Deus Kibamba, Mhadhiri wa Masuala ya Diplomasia na Mjumbe wa Umoja wa Wadau wa Kupata Habari (CoRI), alibainisha hayo wiki iliyopita alipozungumza katika kipindi cha Kipima Joto cha Kituo cha Runinga cha ITV.

Kimbamba alikuwa anajibu swali la Isaac Mpayo, mtangazaji wa kipindi hicho aliyehoji wadau wa habari wanahakikishaje muswada huo unafika na kueleweka kwa wananchi. "Tutakaporejea kutoka katika kuuchambua, hautakuja katika maneno haya magumu ya Kiingereza, utakuja kwa maneno laini ya Kiswahili.

"Hivi sasa kikosi chetu kinafanya mkakati kulainisha ili tuweze kutoa hoja katika lugha ya Kiswahili ambayo wananchi wanaweza kuifikia," alisema.

Kibamba ambaye ni mwandishi wa habari mzoefu alisema kuwa awali wananchi na wadau wa habari walipendekeza miswaada iwe inawasilishwa kwa lugha mbili tofauti (Kiswahili na Kingereza) na sio lugha moja ya Kiingereza kama ilivyo sasa.

"Miswada hii wananchi na sisi wadau tumewahi kupendekeza iwe inatoka katika mtindo ambao unaweza kusambaa vizuri kwa wananchi.

"Kwa mfano, Mama Anna Makinda alipokuwa Spika, Bunge liliwahi kuridhia hoja ya miswada iwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili," alikumbusha.

Alisema CoRI inao wajibu wa kuhakikisha maudhui ya muswada huo yanawafikia wananchi ikiwa ni pamoja na kuandika habari fupi, pia uchambuzi wa makala kwa lugha laini inayoeleweka kwa wananchi.

Katika kipindi hicho, Deodatus Balile ambaye ni Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), alisema CoRI imeunda kamati ya watu sita ambao kwa pamoja watapitia na kuuchambua Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Habari uliosomwa bungeni kwa mara ya kwanza mwezi huu.

"Umoja wa Wadau wa Kupata Habari tumekutana, tukaunda kamati ya watu sita ambayo nimo kwenye hiyo kamati, kwamba twende tuuchambue kwa kina ili twende hatua inayofuata.

"Si yote yaliyopita tuliyokuwa tumependekeza, lakini si yote yaliyobaki. Yaani kuna mabadiliko makubwa yaliyotokea. Mfano, wameondoa kashfa kuwa jinai. Sasa hatutaona mtu anasema 'umemsema vibaya waziri'. Ninafikiri hili tuwapongeze serikali," alisema.

Joyce Shebe, mmoja wa wahariri wa Kituo cha Runinga cha Clouds, alisema kusomwa kwa mara ya kwanza muswada huo bungeni kunatoa fursa kwa wadau wa habari kuendelea kutoa mawazo yao na kushirikishwa pia.

"Tunarudia tena kusema kwamba huu si muswada wa wanahabari pekee, ni muswada wa Watanzania wote kwa sababu mwananchi anahitaji taarifa, na sisi ndio tumeshikilia dhamana ya kuwapa taarifa lakini serikali naye ni mdau wa habari," alisema Shebe.




Meneja Uhusiano kwa Wanahabari wa Kampuni ya Mawasiliano ya Studiored Public Relations Ltd (SRC), Hilton Mpondela (kushoto), akipokea tuzo ya kampuni bora ya PR nchini kutoka kwa Mhadhiri wa UDOM, Mauya Mbilinyi, walioshinda kwenye tuzo za PR Excellence Awards 2022 zilizoandaliwa na PRST juzi jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM yawaonya wabunge kutisha ma-DC, ma-DED

**Na Thobias Mwanakatwe, SINGIDA**

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida, Martha Mlata, amewaonya wabunge wa mkoa huo dhidi ya tabia ya kuwazonga na kuwatishia wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri badala yake wafuate utaratibu kama kuna matatizo.

Martha alitoa kauli hiyo jana kwenye kikao maalum cha Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Singida ambacho kilipokea taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi kwa kipindi cha miezi sita kuanzia Julai hadi Desemba 2022 iliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba.

"Wabunge fanyeni kazi, acheni kuwazonga, kuwatishia na kuamrisha ma-DC (wakuu wa wilaya) na wakurugenzi. Hakuna kutishia hapa, mimi ndio mwenyekiti, ninawaomba mkifanya kazi vizuri na mimi nitawapa ushirikiano tunachohitaji CCM iendelee kushika hatamu, hatutaki mtu atukwamishe," aliagiza.

Martha alisema watendaji wanaopelekwa mkoani humo ni kwa ajili ya kusaidia mkoa usonge mbele, hivyo wanastahili ushirikiano ili watekeleze vyema Ilani ya CCM.


"Mbunge kama ukifanya kazi yako vizuri, hakuna atakayekutoa, watendaji wameletwa kwenye mkoa wetu kutusaidia, tuwapokee na tuwape ushirikiano ili watusaidie na mkoa wetu usonge mbele lakini kama kuna kirusi kitoke," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema wabunge wanapaswa kutambua kuwa kama kuna matatizo, upo utaratibu wa kufuatwa, akiahidi kukaa na wabunge, wakurugenzi wa halmashauri, wenyeviti wa halmashauri na viongozi wa chama ili kuwekana sawa kuhusu changamoto iliyoko.

Onyo hilo linakuja baada ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Serukamba kueleza kuwa wapo baadhi ya wabunge wanaokwamisha wakuu wa wilaya kwa kuingilia majukumu yao.

"Wabunge niachieni ma-DC wangu wafanye kazi, haiwezekani wewe mbunge unaleta fedha za mfumo wa jimbo halafu hapohapo unaomba uingiziwe kwenye akaunti yako binafsi," alifafanua Martha.

**KABWELA** — **Na Fadhili Mohammed**





Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Singida, Martha Mlata, akisalimia wanafunzi wa Shule ya Sekondari Sekutule Halmashauri ya Wilaya ya Singida DC baada ya kamati ya siasa ya mkoa kutembelea shule hiyo. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Walimu wapigwa 'stop' magari ya wanafunzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto, mkoa wa Dodoma umepiga marufuku walimu wa kiume kusindikiza magari ya shule (school bus).

Katika kutekeleza hiyo, imeagizwa kuwa kuanzia sasa wanawake pekee ndio watakaohusika na jukumu hilo la kusindikiza wanafunzi wakati wa kutoka nyumbani kwenda shuleni na kurudi.

Marufuku hiyo ilitolewa juzi kwenye kikao kilichoratibiwa na Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, kilichojumuisha walezi wa vituo vya kulelea watoto (day care), walezi wa makao ya watoto, wamiliki wa shule na vituo hivyo kutoka halmashauri zote za mkoa.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Dodoma, Josephine Mwaipopo, akizungumza na waandishi wa habari baada ya kikao hicho, alisema lengo ni kuwajengea uwezo walezi na wamiliki wa makao ya watoto pamoja na vituo vya kulelea watoto kuhusu sheria, miongozo na kanuni za nchi.

Alisema pamoja na kuwajengea uwezo, kikao hicho kimehitimishwa kwa kuwekwa maazimio mbalimbali, wakiwamo walimu wa kike kutumika kusindikiza magari ya shule badala ya wanaume.

"Kikao hiki kimehusisha zaidi ya walezi na wamiliki 200 na mwisho tumekuja na maazimio kwamba walimu wa kiume kuanzia sasa hawataruhusiwa kusindikiza magari ya shule. Watakaotumika ni walimu wa kike na tunapanga kuona ni jinsi gani hata madereva ambao watatumika kuendesha hiyo 'school bus' wawe wanawake pia.

"Siyo kama hatuwaamini walimu wa kiume tena lakini kutokana na tabia za wanaume wachache, zimeharibu sifa za wanaume wengine, hivyo kuanzia sasa mkoani kwetu walimu wa kike ndio tutawatumia ili kupunguza matukio haya ya ukatili kwa watoto hasa katika vitendo vya ulawiti pamoja na unajisi," alisema Mwaipopo.

Pia alisema azimio lingine ni kwa vito vyote vya kulelea watoto pamoja na makao ya watoto ambavyo havijasajiliwa vifanye hivyo ndani ya miezi mitatu na baada ya hapo hatua za kisheria zitachukuliwa.

Alisema zaidi ya asilimia 60 ya vituo vya kulelea watoto na makao ya watoto havijasajiliwa, hivyo kuendeshwa kinyume cha sheria, kanuni na miongozo ya nchi. "Tumekubaliana kwa pamoja hivi vituo vyote pamoja na makao ya watoto ambavyo bado havina usajili wa serikali kukamilisha usajili ndani ya miezi mitatu na baada ya hapo atakayeshindwa kutimiza maelekezo hayo tutamfungia kutoa huduma," alisema Mwaipopo.

Kadhalika, alisema wamekubaliana kila robo ya mwaka watakuwa wanakutana kujadiliana fursa na vikwazo pamoja na kutathmini maadhimio waliyojiwekea. "Lakini katika kikao hichi pia tumewafundisha walezi kuacha kutumia nguvu kuwafundisha watoto wadogo kwa kuwa umri wa kuanzia mwaka sifuri hadi miaka nane wanajifundisha kwa njia za fahamu hivyo ni bora wakawaacha wajifunze kwa kusikia, kuona pamoja na kucheza ili wasiharibu ubongo wa watoto," alisisitiza Mwaipopo.

Hata hivyo, alizitaka shule pamoja na vituo hivyo kuripoti matukio ya ukatili wa kijinsia ndani ya saa 24 kila yanapotokea na atakayeshindwa kufanya hivyo atachukuliwa kama sehemu ya ukatili huo.

"Toeni taarifa kila matukio ya ukatili yanapotokea kwenye maeneo yenu, kuna mtu anaweza kusema anaogopa kuharibu taswira ya shule yake lakini tukibaini kuwa umeficha taarifa tutakuchukulia hatua kwa mujibu wa sheria," alisema.

# Wananchi walia ukosefu wa maji

**Na Steven William,** MUHEZA

WANANCHI wa mji wa Muheza, mkoani Tanga, wameomba serikali kuwasaidia kutatua uhaba wa maji kutokana na kukosekana kwa huduma hiyo, hivyo kuwalazimu kutumia maji ya chumvi hali inayowalazimu kununua dumu lita 20 kwa Sh. 1,000.

Mmoja wa wakazi wa mji wa Muheza, Aziza Omari, alisema juzi kuwa wanalazimika kutafuta maji ya chumvi katika visima ambayo si salama.

"Kilio chetu kikubwa hapa kwetu uhaba wa maji. Ni kweli kuna changamoto nyingi lakini hizo angalau kidogo tunao uwezo wa kuzitatua wenyewe lakini kwenye shida ya maji, hili limetuzidi uwezo. Ombi letu kwa serikali itusaidie ili tuwe na maji ya uhakika," alisema.

Alisema wananchi walikuwa wanapata maji ya bomba ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA) mara moja kwa wiki lakini kwa sasa hayatoki kutokana na hali ya ukame iliyoko.

Naye Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kwa Antony, Kijiji cha Kigongomawe, Paschal Chalo, alisema uhaba wa maji ni tatizo kubwa linalosababisha maisha kuwa magumu kwa kuwa wanatakiwa kununua kila wakati, hivyo wanaiomba serikali kuwachimbia visima ili wapate maji baridi.

Meneja wa Tanga UWASA wilayani Muheza, Ramadhani Nyambuka, alisema wamepokea ombi la wananchi hao na kwamba wanalifanyia kazi kwa kushirikiana na Mbunge wa Muheza, Hamisi Mwinjuma, ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma.

# Mwenyekiti ataka watendaji kutulia katika maeneo ya kazi

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Chalinze Wilaya ya Bagamoyo, Hassan Mwinyikondo, amewataka watendaji wa kata kukaa kwenye maeneo yao ya kazi kuhudumia wananchi ili kuleta ufanisi wenye tija.

Mwinyikondo alitoa maagizo hayo jana wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri. Pia alimtaka kila mtumishi kusimamia maadili ya kazi yake ikiwamo kuishi kwenye eneo alilopangiwa.

"Mtendaji yeyote hataki kukaa eneo lake la kazi, hatoshi kuendelea kufanya kazi Chalinze. Sisi tunaamini ukiwa karibu na wananchi ni rahisi kushughulikia kero zao kwa sababu watakupata kwa wakati wanapokuhitaji," alisema.

Pia alisema watendaji hao pia watapimwa kulingana na watakavyokuwa wanashughulikia kero za wananchi kwa kipindi cha miezi mitatu na ikibainika hakuna alichofanya, kuna hatua zitachukuliwa dhidi yao.

Awali, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri, Juma Mpwimbwi, aliiomba halmashauri hiyo kutatua kikwazo cha kukosekana kwa mwalimu wa kike kwenye Shule ya Msingi Kwaikonje.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chalinze, Ramadhani Possi, aliahidi kupeleka walimu wa kike kwenye shule hiyo ndani ya siku tatu.

Diwani wa Vigwaza, Mussa Gama, alisema kata yake inakabiliwa na ukosefu wa barabara za mitaa, uhaba wa watumishi wa kada ya afya na uwepo wa migogoro ya wakulima na wafugaji.





# Apigwa faini ya 500,000/- kwa kukutwa na dawa za kulevya

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, imeamuru mkazi wa Olasiti, jijini Arusha, Hadija Sumaye (40), kulipa faini ya Sh. 500,000 au kutumikia adhabu ya kifungo cha miezi mitatu jela, baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kukutwa na dawa za kulevya.

Mshtakiwa huyo, alitiwa hatiani juzi na kuhukumiwa adhabu hiyo baada ya kukutwa na kilogramu 1.5 za mirungi akiisafirisha kwa kutumia basi la abiria.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Victor Kimario, alisema mshtakiwa ametiwa hatiani baada ya kukiuka kifungu cha 17 (1) (b) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2005 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019.

Kwa mujibu wa Hakimu Kimario mwenendo wa kesi hiyo unaonyesha kuwa mshtakiwa baada ya kufunguliwa mashtaka katika kesi namba 127 ya mwaka 2022, alikiri mbele ya mahakama hiyo kosa hilo, baada ya kusomewa hoja za awali juu ya shtaka linalomkabili.

"Kwa kuwa mshtakiwa amekiri kosa mbele ya mahakama hii, mahakama imelitazama shtaka linalomkabili na imeona alikuwa na kiasi kidogo cha dawa hizo. Hivyo ina mhukumu kulipa faini ya shilingi 500,000 au kwenda jela miezi mitatu," alisema.

Baada ya kumalizika kusomwa kwa hukumu hiyo, mshtakiwa alifanikiwa kulipa faini hiyo na kuachiwa huru na mahakama hiyo.

Awali, kabla ya Hakimu Kimario kusoma hukumu hiyo, Wakili wa Serikali, Peter Utafu, aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali ili iwe fundisho kwa watu wengine.

Alidai kuwa adhabu kali ikitolewa kwa mshtakiwa, itasaidia kulinusuru kundi la vijana, ambalo liko kwenye hatari ya kuathiriwa na dawa za kulevya.

Alipopewa nafasi ya kujitetea ili kupunguziwa adhabu, mshtakiwa Hadija Sumaye, aliiomba mahakama hiyo kumpunguzia adhabu, kwa kuwa ana familia inamtegemea.

# Shirika lakabidhi madarasa mawili Longido

**Na Daniel Sabuni,** LONGIDO

SHIRIKA la World Vision Tanzania kupitia mradi wa maendeleo wa Ketumbeine AP limejenga madarasa mawili katika Kijiji cha Lengai na kuwapunguzia kadhia watoto wa Kimasai wanaotoka kijiji hicho kutembea kilomita 25 kufuata masomo katika Shule ya Msingi Loondolwa iliyoko Kijiji cha Loonduo-Esirwa mkoani Arusha.

Kabla ya kutekelezwa mradi huo, wanafunzi wengine wa jamii hiyo kutoka Kijiji cha Gilai Merugoi, Tarafa ya Ketumbeine, nao walikuwa wakienda kufuata masomo Kijiji cha Gilai Bomba, umbali wa kilomita 10, lakini baada ya ufumbuzi wa tatizo hilo, sasa wanatembea wastani kilomita nane mpaka 12.

Akizungumza jana katika Shule ya Msingi Loondolwa, wakati wa hafla ya kukabidhi vyumba viwili vya madarasa yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 90 pamoja na ofisi ya walimu, Mratibu wa Mradi wa Maendeleo wa Ketumbeine AP, Peruth Daud, alisema mradi huo umeigharimu Sh. milioni 74.7.

"Fedha za kutekeleza mradi huu ni msaada kutoka Shirika la World Vision Ujerumani. Uamuzi wake unaangalia zaidi kupunguza ukatili wa kingono dhidi ya wanafunzi, hasa ndoa, mimba za utotoni na utoro.

"Ukitazama ripoti nyingi za elimu katika ukanda huu utaona kwamba wasichana wengi wa jamii ya Kimasai hukatisha ndoto zao kutokana na matatizo haya. Kwamba ndoa na mimba za utotoni kwa watoto wa kike katika maeneo ya jamii hii, huchangiwa na umbali mrefu wa kutoka nyumbani kwenda shule." Alisema kukamilika kwa mradi huo kutapunguza matukio ya ndoa za utotoni pamoja na mimba kwa kiwango kikubwa kwa sababu umbali wa kutembea kwenda shule umepungua na dalili ni idadi kubwa ya watoto kuandikishwa na kuhudhuria shule.

"Tuliguswa kutekeleza mradi huu, baada ya wanakijiji kuwasilisha ombi maalum World Vision Tanzania, ndipo na sisi tukawasiliana na World Vision Ujerumani kuwaomba kutuunga mkono na wakakubali ujenzi ukaanza Desemba mwaka 2022 na kukamilika Februari 2023," alisema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Loondoluo, Keton Ngairugoi, alisema kukamilika kwa mradi huo kutapunguza matatizo ya watoto kwenye kijiji chake na pia kusaidia kupata nafasi ya kuendelea na masomo, kwa kuwa kijiji hicho kina wakazi 9,806 na kaya 1,026 ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Mkuu wa Shule ya Msingi Loondolwa, Lepilal Mollel, alisema shule hiyo ilianzishwa kama shule shikizi, chini ya Shule ya Msingi Gilai Bomba na baadaye ilisajiliwa kuwa Shule ya Msingi Loondolwa, mwaka 2020.

Mollel, alitaja na kushukuru miradi iliyokwishatekelezwa kuwa ni tangi la maji, lenye ujazo wa lita 5,000, kugawa chakula cha wanafunzi, kugawa mbuzi 82 na kondoo 60, ng'ombe, mafunzo ya ufundi stadi kwa vijana wawili na kutoa chanjo kwa watoto walio chini ya umri wa miaka 0-5, mara kwa mara.

Baada ya makabidhiano ya mradi huo, Mkuu wa Wilaya ya Longido, Marco N'gumbi, alitaja World vision Tanzana kama mkono wa pili wa serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Alisema shirika hilo limetekeleza miradi ya shilingi milioni 227 katika kipindi kifupi kutokana na maeneo mengi ya Tarafa ya Ketumbeine, kukumbwa na ukame, ambao umekuwa ukiathiri familia na hasa watoto kutokana na kutegemea mifugo.



Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT), Kata ya Songe, Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga, Amina Lusewa, akishiriki kupanda miti kwenye eneo la ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Kigua katika kijiji cha Kwamba. **PICHA: DEGE MASOLI**

# RC awatangazia 'vita' wanaotumia vyandarua kufugia kuku, samaki

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba, amewanyooshea 'kidole' wananchi wanaotumia vibaya vyandarua vya msaada vinavyotolewa kwa ajili ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa malaria.

Amezionya baadhi ya familia zinazotumia vyandarua hivyo, kama nyumba za kufugia kuku na miundombinu ya kuvulia samaki katika Bahari ya Hindi na mabwawa.

Alitoa onyo hilo jana jijini Tanga, wakati wa uzinduzi wa ugawaji wa vyandarua kwa wanafunzi wa shule za msingi 1,083 zilizoko mkoani humo.

"Nawaagiza viongozi wote wa serikali, dini na jamii, kusimamia matumizi sahihi ya vyandarua hivi.

Jamii ielimishwe umuhimu na matumizi sahihi ili kuepuka matumizi yasiyotarajiwa, kama tulivyoshuhudia kwenye mipango mingine iliyopita.


"Walimu shuleni kwa kushirikiana na wataalamu wa afya, mtoe elimu na kusisitiza matumizi sahihi ya vyandarua hivi, kwa wanafunzi wakati wa ugawaji shuleni," alisisitiza Mgumba.

Alisema ili kuhakikisha kiwango cha maambukizi ya malaria kinapungua hadi kufikia asilimia sifuri ifikapo mwaka 2030, serikali kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imeandaa mpango wa ugawaji wa vyandarua vyenye viuatilifu kwa wanafunzi hao kuanzia darasa la kwanza hadi la saba.

Katika hafla hiyo, Meneja wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Mkoa wa Tanga, Siti Abdulrahman, alisema kuwa serikali imewapa jukumu la kusambaza vyandarua hivyo kwa mikoa ya Iringa, Dodoma, Manyara, Kilimanjaro na Tanga.

Alisema kwa Mkoa wa Tanga wamepatiwa vyandarua 529,641 vya Sh. bilioni 2.6 vitakavyogawiwa kwa shule zote za msingi kuanzia mwanafunzi wa darasa la kwanza hadi la saba.

Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashimu Mgandilwa, alisema kwa nafasi yake ana uwezo wa kuingia mahali popote akishirikiana na viongozi wengine wa serikali kuhakikisha wananchi hawaendi kinyume na matakwa yaliyowekwa.








Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi (katikati), akichangia damu katika Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga pamoja askari polisi na wanakikundi cha mazoezi cha Polisi Jamii Fitness Center (PJFCS) jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wasiojulikana wachoma nyumba ya Ofisa Maendeleo

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WATU wasiojulikana usiku wa manane wamechoma moto nyumba ya Ofisa Maendeleo ya Jamii katika Kata ya Ilola wilayani Shinyanga, Bandi Magoye.

Tukio hilo lilitokea juzi wakati ofisa huyo akiwa amelala na familia yake ya watu watano na waliona mwanga sebuleni huku moshi ukiwa umetanda ndani.

Akisimulia tukio hilo, Magoye alisema baada ya kuona moto unawaka ndani walianza kupiga kelele kuomba msaada kwa majirani, huku wakiendelea kuuzima na walipojaribu kutoka nje walishindwa kwa sababu milango ilikuwa imefungwa kwa nje.

Alisema anamshukuru Mungu moto huo haukuleta madhara na kuviomba vyombo vya ulinzi na usalama kufanya uchunguzi ili kubaini wahusika pamoja na kumhakikishia usalama wa maisha yake. "Watu hawa walikuwa wamedhamiria kuniua kabisa kwa sababu tulikuta kangamlangoni imeandikwa bwana alitoa na bwana ametwaa na walishindwa kuingia ndani huenda wangenikata na mapanga," alisema Magoye.

"Chanzo cha tukio la mimi kutaka kuchomwa moto ndani ya nyumba, linatokana na kupinga matukio ya ukatili wa kijinsia wananchi wanasema nawaingilia mambo yao, kwamba wao huwa wanamalizana, lakini mimi nayafikisha mbali na kutoa taarifa polisi hivyo hawanitaki nifanye kazi kwenye kata hii," alisema. Alisema wiki iliyopita kwenye mkutano wa hadhara wananchi walisema kwamba kwa kuwa yeye amejenga nyumba kwenye kata hiyo ya Ilola, wanamruhusu aishi, lakini siyo kufanya naye kazi bali ahamie sehemu nyingine. Aidha, alisema kwa sasa ana ugomvi na mume wake na wameshapeana talaka na kwamba amekuwa akimpigia simu za mara kwa mara ambazo hazina ujumbe mzuri na kuomba vyombo vya usalama vifanye uchunguzi.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wilayani Shinyanga, Aisha Omary, alilaani tukio hilo la kuchomwa moto nyumba hiyo na kuomba sheria ichukue mkondo wake kwa wahusika wote ambao walifanya jaribio hilo la mauaji.

Mkuu wa Divisheni ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, David Rwazo, alisema ripoti ya uchunguzi ikitoka na kuonekana hakuna usalama wa ofisa huyo, menejimenti itakaa na kuona namna ya kufanya.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Imalanguzu, Onesmo Mashimba, alisema yeye alikuwa mtu wa pili kufika eneo hilo la tukio na kubainisha kuwa tayari wameshakaa na uongozi wa Jeshi la Jadi na kukubaliana kumpatia ulinzi wakati uchunguzi ukiendelea ili kuwabaini wahusika.

Alikiri ni kweli wananchi walimkataa ofisa huyo kuendelea kufanya kazi kwenye kata hiyo pamoja na Mtendaji wa Kata, Ofisa Kilimo na Diwani kwa madai kwamba wanaingilia masuala yao.

Alisema siku za nyuma ikitokea tatizo wananchi walikuwa wanakaa vikao na kumalizana, lakini wao wanatoa taarifa polisi ambao hufika na kukamatwa watuhumiwa kitendo ambacho hawakitaki.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Janety Magomi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kubainisha kuwa wanamshikilia mzazi mwenzake kwa uchunguzi kwa sababu walikuwa na ugomvi.

# Mbunge aagiza wazazi, wanafunzi kusakwa

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

MBUNGE wa Ilemela, Dk. Angeline Mabula, ameagiza kusakwa na kuchukuliwa hatua kwa wanafunzi saba pamoja na wazazi wao waliotakiwa kuripoti shuleni lakini hadi sasa hawajaripoti. Wanafunzi hao walitakiwa kuripoti katika Shule ya Sekondari Igogwe kuanza kidato cha kwanza. Alitoa amri hiyo mwishoni mwa wiki alipotembelea shule hiyo ikiwa ni sehemu ya kukagua shughuli mbalimbali jimboni humo. Alisema baadhi ya wanafunzi hao baada ya kumaliza darasa la saba walitoroka nyumbani, huku wengine wakiwa wameolewa.

Katika ziara hiyo alikagua utekelezaji wa miradi ya kupunguza umaskini ikiwamo ujenzi wa bweni la wasichana katika shule hiyo.

Alisema katika shule hiyo ilipangiwa wanafunzi 167 wa kidato cha kwanza kwa mwaka wa masomo 2023 na kati yao 160 wameripoti shuleni, huku saba 'wakikacha' na sababu zimeelezwa kuwa baadhi yao wameolewa na wengine walitoroka nyumbani.

"Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya hao watoto saba na wazazi wao lazima wapatikane kama kushtakiwa anashtakiwa mzazi na mtoto, haiwezekani Rais anatoa fedha za kutosha kwa ajili ya kuweka miundombinu Sh. milioni 516 kwa kata moja, lakini wao hawajaripoti shule," alisema Dk. Mabula.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Igogwe, Atanas Manyika, alisema kuwa shule hiyo kwa mwaka wa masomo 2023, ilipangiwa wanafunzi 167 wa kidato cha kwanza, lakini mpaka sasa wameripoti wanafunzi 160.

# Manispaa kugawa vyandarua shuleni kudhibiti malaria

**Na Restuta Damian,**
BUKOBA

MANISPAA ya Bukoba mkoani Kagera imepanga kugawa vyandarua katika shule za msingi zote ili kukabiliana na ugonjwa wa malaria.

Pia wamepanga kati ya mwaka 2025/2030 maambukizi ya ugonjwa huo yapungue hadi asilimia moja.

Hayo yalisemwa na Mganga Mkuu wa Manispaa ya Bukoba, Dk. Peter Mkinda wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema tayari hatua ya kwanza ya kugawa vyandarua kwa mama wajawazito na watoto chini ya umri miaka mitano wakiwa katika zahanati na vituo vya afya kupata huduma imeanza.

Alisema njia nyingine iliyotumika kwa mwaka jana hadi sasa ni kugawa vyandarua kwa wanafunzi wa madarasa ya awali wakiwa shuleni ili wavipeleke nyumbani.

"Njia hizo mbili tunaamini kwamba familia ina baba, mama na watoto, hivyo kati yao tumeona kundi la watoto na mama ni wepesi kukubali na kutumia vyandarua," alisema Dk. Mkinda.

Aidha, alisema Mji wa Bukoba kuna mbu wakati wa mvua kutokana na kuwapo majani mengi na madimbwi wakati wa masika.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita maambukizi ya ugonjwa huo yamepungua na kufikia asilimia 5.4 kutoka asilimia 7.0.

Daktari Kiongozi kutoka Kituo cha Afya cha Zamzam, Dk. Godphas Kaegeji, alisema wajawazito na watoto wa chini ya miaka 14 ni miongoni mwa makundi yanayoshambuliwa na malaria.

Alisema ugawaji wa vyandarua kwa kundi hilo umefikia asilimi 86 na mwaka jana waligawa kwa wanafunzi 1, 500 wanaosoma darasa la pili kwa baadhi ya shule katika Manipaa ya Bukoba.

Nipashe
# TESA
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI
Jumanne Februari 21, 2023

## Mlango unaowainua wasichana kwenye sayansi unapofunguka




Ukurasa 14

Vita vilivyosheheni vifaa vya kielektroniki



Ukurasa 13

ELIMU

NA PANCRAS LUOGA

# Makonda daladala kwa mateso haya wanazalisha kizazi hatari



KILA mara asubuhi na jioni hekaheka za wanafunzi wa shule za msingi na sekondari walio kwenye harakati za kwenda shuleni au kurudi nyumbani zinaongezeka, utawaonea huruma.

Ni huruma ambayo pia huwapata wazazi na walezi pamoja na jamii kutokana na changamoto ya wanafunzi kukataliwa, kukemewa, kutukanwa na muda mwingine kushushwa kutoka kwenye vyombo vya usafiri.

Wakati hayo yakifanyika kila mmoja akumbuke kuwa wengi wao ni watoto wenye umri wa chini ya miaka 18 ambao kwa miaka hiyo miili na akili zao bado hajaweza kustahimili usumbufu huo ambao sio wa lazima.

Hivyo suala hili linawafanya baadhi ya wanafunzi hao kupata madhara ya kiafya kwa muda na pengine wakati mwingine bila wenyewe wala wazazi au walezi kujua. Huenda ni kwa sababu madhara yake hayatokei kwa siku moja ila hujitokeza baada ya muda mrefu wa kuendelea kukataliwa, kugombezwa na kufokewa na kushushwa toka vyombo vya usafiri na wakati mwingine kuambiwa wewe mtoto kaa pembeni wapishe wakubwa.

Si kwenye dala dala pekee, mtoto anawekwa pembeni kwenye foleni za maji bombani, kwenye vibanda vya chips, mitaani hata kwenye migahawa na huduma karibu zote za kijamii. Cha ajabu ni kuwa jamii imekuwa ikishuhudia vitendo hivyo vyote vikitokea katika maeneo mbalimbali hasa stendi za kusubiria, kushukia usafiri hasa daladala bila kuchukua hatua hata kukemea changamoto hiyo.

Mwanafunzi akitaka kupanda daladala kondakta anawaambia kuwa muda huu sichukui wanafunzi au kama huna hela ndogo kuanzia Shilingi 200, 100 au 50 zilizotosheleza usipande gari. Kibaya zaidi akitoa hela kubwa kwa mfano 2,000 au 5,000 kila mmoja atamwonea, anafokewa na hata kucheleweshewa chenji hata kama kafika kituoni anaposhuka.

Madereva na makondakta wakumbuke kuwa anayetakiwa kulaumiwa si mwanafunzi ila ni mzazi au mlezi wa mtoto, kwasababu ndiye anayetoa hela hiyo na wakati mwingine hupewa hela hizo usiku wa manane au alfajiri ambako hakuna sehemu ya kuomba chenji.

Akipanda kwenye basi atasukumwa na kukaripiwa muda mwingine bila sababu ya msingi, akikaa ataambiwa awapishe wakubwa asimame. Wengine dereva anawaruhusu wakae wawili kiti kimoja akija kondakta anawafokea kwanini wanakaa.

Kwa ujumla wanafunzi wamekuwa wanyonge mno kwenye vyombo vya usafiri na kila mmoja aamke kuanzia sasa achukue nafasi ya kuwa mzazi au mlezi na kuwasaidia.

**ATHARI UNYANYASAJI**

Kuna madhara mengi yatokanayo na vitendo vya wanafunzi kukataliwa, kusukumwa na kunyanyaswa kwenye vyombo vya usafiri. Baadhi yake ni kuleta matatizo ya mbalimbali ya kiafya.

Yanaweza kujitokeza na kuanza kuonekana katika kipindi kifupi japo nyingi ya athari hizo hujitokeza baada ya muda mrefu. Pia watoto hawa huanza kujengeka na kuwa mitazamo hasi dhidi ya jamii kwa kuona kuwa haiwasidii wanapokuwa na changamoto katika maisha na shughuli zao.

Wapo wanaojiandaa kulipiza kisasi, hata ukubwani na wapo wanaopata matatizo ya afya ya akili. Kwa mfano, wanafunzi wengi kukosa hali ya kujiamini na kupata matatizo ya msongo wa mawazo na hofu wakati mwingine.

Zaidi madhara haya makubwa ya kiafya yanayotokana na vitendo vya kugombezwa na kubezwa ovyo, kukataliwa na kunyanyaswa kila siku na wahudumu wa vyombo ya usafiri na kwenye huduma za kijamii mara nyingi si rahisi kuyatibu. Pia hutumia muda mwingi sana kuyatibu huku hakitumia fedha nyingi katika matibabu yake.

Pia watoto hawa hulazimika kuwa na ujeuri, lugha mbaya hata matusi kutokana na kukerwa na kuchoshwa na jamii wanayooishi kwenye vyombo vya usafiri.

Sote ni mashahidi jinsi wanafunzi wanavyopata shida kwenye nyombo vya usafiri hasa muda wa asubuhi na jioni ambayo huwa ni muda wa abiria wengi kwenda au kurudi kutoka maeneo wanayotafutia riziki.

**CHA KUFANYA**

Kwanza kila mtu atambue kuwa usafiri kwa wanafunzi ni muhimu ili kufika shuleni kwa wakati na kuweza kumudu masomo.

Na kwa kuzingatia mantiki hiyo ni lazima kuwasaidia wanafunzi kuondokana na usumbufu huo. Pili, wanajamii ambao ni wazazi au walezi ama ndugu pamoja na marafiki na serikali ni lazima kuchukua hatua kukemea badala ya kukaka kimya.

Wanaofanyakazi kwenye vyombo vya usafiri wajitahidi kuwathamini wanafunzi na kuona kuwa nao ni binadamu na wanaweza kuwa sawa na watoto wao hivyo wanahitaji kupendwa na kusaidiwa.

INAENDELEA UK. 12

ELIMU

**NA SABATO KASIKA**

# Juhudi kutokomeza ukatili kijinsia zilivyovuna sifa kitaifa, kimataifa

UELEWA mdogo kuhusu madhara yatokanayo na ukatili wa kijinsia ni miongoni mwa sababu zinazotajwa kuchangia kuendelea kuwapo kwa vitendo hivyo.

Serikali na wadau wanaendelea kutoa elimu kuhusu athari za ukatili wa kijinsia mashirika ya kijamii yakiwa mstari wa mbele.

Miongoni mwa wadau hao, ni Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni Dar es Salaam, ambacho hivi karibuni kinapokea wadau kutoka mataifa ya kigeni wanaovutiwa na mbinu wanazotumia kufikisha elimu kwa umma.

Wageni hao wanatoka Ireland, Palestina, Uingereza na Sierra Leone wanaoongozwa na Ubalozi wa Ireland Tanzania, ili kujionea mafanikio ya kituo hicho, katika utoaji wa elimu ya kupinga ukatili huo.

Akizungumza katika ziara hiyo, Ofisa Maendeleo ya Jamii Mwandamizi kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dorah George anakisifu kwa kazi ya mfano.

"Kituo kimetembelewa kutokana na juhudi zake binafsi za kufanya kazi za maendeleo ya jamii, kwa njia shirikishi kwa maana ya kushirikisha makundi mbalimbali na kuwavutia wageni hawa kukitembelea," anasema Dorah.

Anaeleza kuwa mashirika yasiyo ya kiserikali yanayotoa elimu ya kupinga ukeketaji ni mengi na kuwapa kwamba Kituo cha Sauti ya Jamii ni mojawapo wa mfano wa kuigwa na kimewafanya wadau kutoka nje kuja kujifunza kitu.

Kiongozi wa msafara wa wadau hao walifika katika kituo hicho, Mkuu wa Idara ya Jinsia kutoka Serikali ya Ireland, Tom Crowley anasema ujuzi waliopata kituoni hapo wataufikisha katika maeneo mengine duniani.

"Tumekuja hapa kutoka mataifa mbalimbali, tumejifunza jinsia wanavyotoa elimu ya kukabiliana na ukatili wa kijinsia, nasi tumepata ujuzi tutaufikisha kwa wengine nao waige mfano wenu," anasema Crowley.

Mkuu wa Idara ya Programu ya Ruzuku kutoka Women Fund Tanzania (WFT), Redimna Ginwas, anasema Ireland huwawezesha kifedha ambazo wao hufadhili vikundi vinavyopambana na ukatili wa kijinsia.

"Wafadhili wameridhika na kazi yenu ya kupambana na ukatili wa kijinsia katika jamii, hivyo tunawatia moyo mwendelee zaidi ili kuhakikisha jamii inaishi salama bila ukatili wa aina yoyote," anasema Redimna.

**WALIVYOANZA**

Katibu wa Kituo cha Sauti ya Jamii, Sada Shifta, anasema mwaka 2014, walianza kazi kwa kuita watu katika kituo hicho na kuwapa elimu kuhusu haki zao na kuwahamasisha kukataa vitendo vya ukatili.

"Baadaye tukaanza kwenda kwa wanajamii na baada ya kuona mwitikio mkubwa watu wanaotamani kupata elimu hii, na tumefanikiwa kufikia wengi, ingawa vita zaidi inahitajika," anasema Sada.

Anaeleza kuwa kwa njia hiyo, wamesaidia baadhi ya mabinti kupata mafunzo ya chereheni na ujasiriamali, hasa wale waliokimbia vitendo vya ukeketaji kutoka nyumbani kwao baada ya kuelimika na kutambua madhara ya ukatili huo.

"Kuanzia mwaka 2017 hadi 2022 tumefikia watu 1,111, wanawake ni 895 na wanaume 216. Aidha, mafunzo ya ujasiriamali kwa vitendo tulifikia watu 5,842 lakini tukiwaokoa mabinti 109 kutoka mikono ya wakeketaji," anasema.

Kipunguni ni eneo linaloishi jamii za wakeketaji wanaoendeleza mila na desturi hizo.

Kadhalika katika kipindi chote hadi sasa, wamefanikiwa kuongeza hamasa ya kudai haki na kwamba wananchi wamefunguka wanaripoti vitendo vya ukatili ikiwamo rushwa ya ngono anasema.

Anatoa mfano kuwa mwaka 2014 vitendo vya ukatili vilikuwa haviongelewi wala kuripotiwa, lakini kwa sasa wanapokea kesi nne hadi saba kwa siku, wanaume wanashiriki mijadala ya ukatili, wanawake na wasichana wanaripoti vitendo vya rushwa ya ngono.

Anafafanua kuwa kituo kimeongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi na kwamba wamekuwa na jamii inayochukua hatua juu ya vitendo vya ukatili huku wakiwa na viongozi wa serikali bega kwa bega.

"Tumeanzisha klabu za kupinga ukatili ndani ya jamii, baadhi ya ngariba na wazee wa mila wameacha ukeketaji, lakini elimu tunayoitoa, imesaidia kuongeza uelewa wa haki kwa wafanyakazi wa majumbani," anasema.

Mkurugenzi wa kituo hicho, Seleman Bishagazi anatoa ombi kwa WFT kuendelea na utaratibu wa kutoa ruzuku bila kuzingatia vikundi vya watu wenye elimu kubwa katika ufadhili bali hata wa kawaida wanaoishi karibu na jamii.

"WFT wanatoa fedha kwa vikundi vya kujamii kama chetu, lakini mashirika mengine yanaangalia elimu za watu badala ya kazi zinazofanywa na yanatoa fedha katika asasi si kwa vikundi," anasema Bishagazi.




Annapili Ngome (wa tatu kushoto), kutoka Taasisi ya Kaya Foundatiom akiendesha darasa. PICHA ZOTE: SABATO KASIKA




Mmoja wa Maofisa wa Ubalozi wa Ireland Tanzania, Oliva Kinabo, akichangia hoja katika mafunzo hayo.

# Makonda daladala kwa mateso haya wanazalisha kizazi hatari

INATOKA UK. 11

Hivyo wasiwanyanyase, kuwakataa na kutukana. Zaidi, kila mmoja akumbuke kuwa wanafunzi hawa ndiyo Tanzania ya kesho hivyo wasipande mbegu mbaya kwani kesho itakuwa kubwa na kuleta madhara kwa jamii.

Aidha, baada ya kuyatambua haya yote, lazima kwa ujumla watu wachukue hatua ya kusaidia watoto hawa dhidi ya changamoto hiyo. Jamii iwasaidie kwa kuongea na kuwakemea wahudumu wa vyombo vya usafiri na popote wanapotenda vitendo vya kuwakatili na kuwaudhi watoto au wanafunzi.

Juhudi zitasaidia watoto na wanafunzi kujisikia kuwa wanathaminiwa na jamii inayowazunguka na pia inawasaidia katika kufikia malengo yao ya kielimu au kupata mahitaji ya kijamii.

Halikadhalika, wanafunzi wataanza kujisikia kuwa wapo salama zaidi katika jamii inayowazunguka hasa linapokuwa suala la usafiri wa kwenda na kurudi nyumbani.

Pili, licha ya kutambua kuwa wazazi au walezi wametingwa sana na majukumu ya kutafuta riziki kwa ajili ya familia na kuchelewa kurudi, wajitahidi sana kuwaandalia watoto wao nauli ambazo ni za chenji ndogo ndogo lakini pia kuwatafutia usafiri mbadala ikiwezekana ili kuwaepusha watoto wao dhidi ya usumbufu.

Na hili ni tatizo kubwa sana hasa muda asubuhi pale mwanafunzi anatotoa noti ya elfu tano au kumi ili kulipa shilingi mia mbili na pengine wazazi/walezi wanaweza kusaidia watoto wao kwa kuwapa hela ndogo ndogo kama wanazo au kutafuta hela hizo mapema ili kuwaepusha.

Wito wangu kwa jamii ni kuwa jamii lazima aanze sasa kuwasaidia watoto wanaoenda shuleni kupata usafiri bila kukataliwa au kugombezwa, hii itasaidia watoto kuona jamii inawapenda, inawathamini na inawasaidia katika kufikia malengo yao ya kielimu.

Hivyo kuwa na afya njema ya akili na kupelekea kufanya vizuri katika masomo yao. Tukumbuke watoto ambao ni wanafunzi wa leo ni taifa la kesho hivyo lazima tujitahidi kuwaandaa na pia kuwalinda dhidi ya usumbufu wa aina yoyote wenye kuweza kuwaathiri kiafya na kushindwa kuja kutoa mchango wao katika ujenzi wa taifa lao.

**Maoni: 0757-645746.**

ELIMU

NA FRANK MONYO

# Mlango unaowainua wasichana kwenye sayansi unapofunguka

## Ni mkakati wasome kozi za uhandisi mitambo, elektroniki na teknolojia

TANZANIA imekuwa mstari wa mbele kuhamasisha wanafunzi wakiwamo wasichana kusoma sayansi, juhudi zikiambatana na ujenzi wa sekondari 'spesho' za wasichana kwa kila mkoa.

Hamasa inaongezeka zaidi awamu ya sita, serikali inapoanza ujenzi wa shule hizo lakini kuanzisha rasmi ufadhili wa vyuo vikuu unaofanikishwa na Samia Scholarships kwa 'vipanga' wanafunzi wanaofanya maajabu kwenye masomo ya sayansi kidato cha sita.

Taifa linalenga na kutamani kuwa na wasomi wa sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati (science, technology, engineering na mathematics-STEM).

Licha ya takwimu za Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), kuonyesha kati ya wanafunzi wote wanaokwenda vyuo vikuu kusoma masomo ya STEM, asilimia 30 pekee ni wanawake.

Ili kuunga mkono juhudi hizo wadau wa elimu, hawajabaki nyuma na katika jitihada za kukabiliana na pengo hilo, Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) inaanzisha mpango wa uanagenzi wa STEM.

Uanagenzi ni mafunzo yanayohusisha kujifunza kutoka kwa wengine na kurithi kwa ufanisi kile wanachokifanya ili kuwa mahiri zaidi.

Ukiwa ni mkakati wa miaka 10 wa Diageo ujulikanao kama Society 2030: Spirit of Progress.

Kupitia mpango wa uanagenzi kwa masomo ya STEM, SBL inafadhili wanafunzi waliohitimu elimu ya juu ili kujifunza na kupata uzoefu muhimu na mafunzo kazini.

Akizungumzia kuhusu programu hiyo kwenye mahojiano na Nipashe, Meneja Ubora wa Uzalishaji wa SBL, Natalia Kimacha, anasema kuna mafanikio ya kujivunia kwenye programu hiyo, hasa jinsi inavyowezesha vipaji katika eneo la sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati.

Anasema kupitia mpango wa uanagenzi kwa masomo ya STEM, SBL inafadhili wanafunzi wanaohitimu elimu ya juu ili kujifunza na kupata uzoefu muhimu na mafunzo kazini.

"SBL kwa wakati wote imekuwa ikisisitiza ushirikishwaji katika shughuli zake za biashara, kwa hivyo, mpango wa uanagenzi wa STEM unaimarisha zaidi dhamira hiyo katika jitihada za kuziba pengo hilo kwa kuwapa wasichana fursa ya kupata ujuzi kwenye masomo ya STEM," anasema Natalia.

Anaongeza kuwa SBL inachukua awamu nyingine ya makundi baada ya kukamilisha awamu ya kwanza ya programu ya uanagenzi.

"Mchakato wetu wa kuajiri huchagua 10 bora kati ya mamia ya waombaji. Tumeunda sera kwa wahitimu na kutoa programu ambayo inawapa uzoefu wa vitendo na nafasi za kazi. Kampuni ina ushirikiano na vyuo vikuu kadhaa na asasi za maonyesho ya kazi." Anaongeza.



Baadhi ya wasichana waliopata fursa ya kupata ujuzi kwenye masomo ya STEM kwa hisani ya SBL. PICHA: MWANDISHI WETU

Natalia anaeleza kuwa mpango wa kampuni ya ufadhili wa masomo ya kilimo ujulikanao kama 'kilimo viwanda' ni mikakati bayana ya jinsi wanavyosaidia vijana kupata uzoefu ndani ya soko la ajira.

Anasisitiza kuwa SBL inaahidi kuendelea kusaidia wanawake katika nyanja za sayansi na teknolojia, kama sehemu ya juhudi zake za kuziba pengo hilo, huku ikipanua mipango yake ya kuwawezesha wanawake katika biashara zake zote pia.

Anawataja wanafunzi ambao wamenufaika na mpango huo baada ya kuhitimu kuwa ni Lydia Masonda, Julieth Masawe na Christina Ndalichako ambao kwa sasa wanafanya kazi kwenye mitambo ya kiwanda cha SBL Moshi.

Akitoa maoni yake kuhusu mpango huo, Lyidia anasema: "Naona fursa ya kukua, pamoja na kupata ajira ya kudumu katika kampuni ya SBL. Ninaweza kusema kwa kujiamini kuwa ninao mustakabali katika safari yangu ya kazi."

Kwa upande wake, Julieth anasema anachukulia uzoefu wake katika programu kuwa safari ya ukuaji kitaaluma na kibinafsi akiongeza:"Sikuwahi kufikiria kwamba siku moja ningeweza kutumia kikamilifu mashine na kuiendesha kwenye uzalishaji tena kwenye kampuni kubwa kama SBL."

"Kuwapo kwangu hapa kunanifanya niwe na ari ya kujifunza na kuwa bora katika ufundi wangu. Nilipata mafunzo ya kiufundi, biashara na upande wa usambazaji wa biashara na vyote vina faida."

Mmoja wa wanufaikaji wa mradi wa STEM kutoka kundi la pili, Miriam Masanja, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, mhitimu wa shahada ya uhandisi wa umeme na elektroniki anasema: "Tangu nijiunge na kundi hili, nimepata ujuzi wa kutatua matatizo na uwezo wa kiutendaji katika kiwanda cha bia."

Halikadhalika anasema amepata ujuzi wa kufanya vitu vingi ambavyo ni zana za maendeleo ya kibinafsi na ukuaji katika sekta hiyo.

Glory Hungu, anayetoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, akisoma shahada ya sayansi ya Chakula na teknolojia na aliyenufaika na mpango wa STEM anasema anaona mpango huo ni muhimu kwa wasichana na wanawake wa taifa hili.

"Siku zote nimekuwa mdadisi wa kutatua changamoto katika masuala tofauti lakini nikiwa na shauku ya kupata ujuzi kupitia majaribio na sayansi daima imekuwa ikinipa majibu ninayohitaji." Anaongeza Glory.

> "SBL kwa wakati wote imekuwa ikisisitiza ushirikishwaji katika shughuli zake za biashara, kwa hivyo, mpango wa uanagenzi wa STEM unaimarisha zaidi dhamira hiyo katika jitihada za kuziba pengo hilo kwa kuwapa wasichana fursa ya kupata ujuzi kwenye masomo ya STEM," anasema Natalia.

TEKNOLOJIA

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Vita vya ‘kisasa’ vilivyosheheni gumzo la vifaa vya kielektroniki

## • Ni vifaru vya Leopards 2, M1 Abrams, Urusi hatihati




Kifaru Leopard 2 kinachosifika kwa ufanisi zaidi ndilo tegemeo la Ukraine kwenye mapambano na Urusi. PICHA: MTANDAO

BAADA ya miezi 12 ya vita kati ya Urusi na Ukraine, kinachoonekana leo si vita ya nipige nikupige bali matumizi ya teknolojia ya zana za kisasa zinazoonyesha ukomavu wa sayansi za kivita kwenye majeshi ya mahasimu na washirika wao.

Gumzo la hivi karibuni ni ujio wa vifaru vya kisasa zaidi kutoka Ujerumani na Marekani kunakotarajiwa kuliongezea nguvu jeshi la Ukraine na kulisambaratisha la Urusi, ambalo kijeshi nchi mbili hizo zinaelekea kuwa na teknolojia na ujuzi wa kivita unaolandana, kwa vile awali yalikuwa mataifa pacha ya Muungano wa Kisoviet.

Vyombo vya Habari vya Magharibi vinaripoti kuwa idadi ya vifaru vilivyokuwa vikitumiwa na jeshi la Ukraine vimepungua kutokana na hasara iliyopata kwa kutandikwa na Warusi.

Vifaru hivyo vinahitajika kuondolewa vitani kutokana na ukosefu wa vipuri vya kuvitengeneza ni kwa sababu idadi kubwa ya silaha za Ukraine kabla ya uvamizi wa Urusi Februari mwaka jana zilitoka Urusi na ndiyo pekee iliyo na vipuri vyake.

Kabla ya vita hivyo, Ukraine ilikuwa na takriban vifaru 900 kutoka Usovieti, kama vile kifaru cha T-72, T-64 pamoja na vile vilivyokuwa vikimilikiwa na mataifa yaliojiunga na Umoja wa Kujihami wa Nchi za Magharibi - NATO baada ya kuondoka Soviet, yaliyoipatia takriban vifaru 200 aina ya T-72.

**VIFARU MATATA**

Vita ya leo ni teknolojia ndiyo maana Ukraine inataka kifaru cha kisasa cha Leopard 2 kinachotengenezwa Ujerumani.

Kifaru cha Leopard ndicho chaguo bora kwa Ukraine, kwani kinatumika sana na kimeenea zaidi kati ya nchi za Ulaya ambazo ni wanachama wa NATO, huko kukiwa na zaidi ya vifaru 2,300 vinavyotumika katika majeshi ya nchi hizo na kinaweza kusafirishwa hadi katika ardhi ya Ukraine kwa ufanisi.

Kifaru hicho kinatumia risasi za NATO, ambazo zinaweza kupatikana kutoka kwa nchi yoyote ya NATO, pamoja na mataifa hayo kuwa na idadi kubwa ya risasi hizo na za vifaru vya Marekani aina ya M1 Abrams ambavyo pia hutumia risasi sawa na Leopard 2, na kwa hivyo Marekani inaweza kutoa risasi za vifaru hivyo na vipuri, ni kwa mujibu wa BBC

> “Kinaweza pia kurudishwa ‘rivasi’ kikimbia kwa maili 19.2 kwa saa takribani kilometa 31 kwa saa kinarudi rivasi na kina uwezo kufanyakazi kwa ufanisi wa kilometa 500 bila kutetereka.

**KIFARU KIKOJE?**

Kwa hivyo ni nini kinachokifanya kifaru kama Leopard 2 cha Ujerumani kuwa silaha inayotafutwa sana kwa vita huko Ukraine?

Maofisa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania wenye utaalamu wa masuala ya vifaru, wanajibu kuwa kifaru ni kama kuweka jeshi zima mkononi mwako, wakimaanisha kuwa kinabeba silaha nyingi na muhimu na nzito na kubwa kwa wakati mmoja kuanzia mabovu, risasi na mizinga pamoja na wapiganaji.

Wakihifadhi majina yao, maofisa hao wanaeleza kuwa kifaru kinaweka pamoja majeshi ya ardhini, anga na majini na mawasiliano.

“Kinashambulia askari wa miguu, kina mizinga inayoangusha ndege, majini kinapiga, kina roketi za kuvunja vifaru vingine, kompyuta na mifumo ya kielektroniki ya mawasiliano. Kwa ujumla kifaru ni kila kitu,” anasema ofisa jina tunalo.

Anaongeza kuwa kifaru kinatembea chenyewe siyo kama mzinga ambao unasafirishwa kwa gari la mizinga. Kina magurudumu ambayo ni mnyororo wa chuma hutembea kwa kasi hupasua msitu, miamba, kwenye vumbi jangwani, kwenye tope hata majini vipo vinavyoitwa ‘amphibians’.

Wanataja uimara wa silaha hiyo kuwa imeundwa kwa umahiri na madini yasiyopenya risasi, mabomu, moto na si rahisi kushambuliwa labda kwa kuweka mabomu mazito ya kulipua vifaru kwenye njia kinapopita, ambayo pengine si rahisi kuitambua.

Kifaru Leopard 2 cha kisasa cha Ujerumani kimethibitishwa kuwa ni kifaa mahiri vitani kuyakabili majeshi ya Urusi, kinasifika kwa kasi ya juu, kikitembea kwenda mbele ni kasi ya takriban maili 42.2 kwa saa takribani kilometa 72.

Kinaweza pia kurudishwa ‘rivasi’ kikimbia kwa maili 19.2 kwa saa takribani kilometa 31 kwa saa kinarudi rivasi na kina uwezo kufanyakazi kwa ufanisi wa kilometa 500 bila kutetereka.

BBC inaeleza kuwa kina uzito wa tani 52 kikiwa tupu na tani 62 kikiwa kimesheheni vifaa vya kivita. Kina uwezo wa kubeba wapiganaji wanne.Ni kifaru kilichoundwa na mchanganyiko wa chuma, mfano ‘tungsten’ na kinaweza pia kuwekewa silaha za msimu au zinazohitajika kwa wakati huo.

Kwa mujibu wa mtandao wa interestingengineering, kifaru cha Leopard 2 kina uwezo wa kuharibu silaha zilizo mbele ya kifaru aina ya T-72 kilichoundwa na Soviet wakati nje unatisha na wa kuogopwa, lakini ufanisi wake kwenye uwanja wa vita unatokana na kuwa na mifumo ya kisasa ya kielektroniki na kompyuta zinazotumiwa kuendesha mapambano kwa ufanisi na umahiri mkubwa.

Unasema zaidi ya hayo, vifaru vya Leopard 2 vinatumiwa na nchi nyingi wanachama wa NATO, tena kuna zaidi ya vifaru 4,000, vikifanya kazi, yote hayo huvipa vifaru hivyo upendeleo huko Ukraine na duniani.

Halikadhalika, mtandao wa runinga ya Aljazeera, unakoleza kuwa vinatumiwa na majeshi ya Austria, Kanada, Chile, Denmark, Finland, Ujerumani, Ugiriki, Uholanzi, Norway, Poland, Ureno, Singapore, Uswizi, Hispania na Uturuki.

Kifaru cha Leopard 2 kiliundwa kwa mara ya kwanza mwaka 1979 na Krauss-Maffei kwa ajili ya Wizara ya Ulinzi ya Ujerumani.

Leopard 2 na vifaru vingine kama Abrams cha Marekani vinafanana ni magari makubwa, yenye silaha nyingi na yamejengwa imara na yana mfumo inayojilinda kikamilifu kuliko kitu chochote kilichojengwa na Wasovieti, au chochote ambacho Warusi wanacho kwa sasa kwenye vita inasema Al Jazeera.

Lakini kinaweza kutengenezwa kutokana na mahitaji ya mteja mfano kinaweza kutembea juu ya maji, kwenye tope, msituni na kinaweza kuwekewa ‘manjonjo’ kuendana na kile jeshi la mteja linachotaka.



# Wanahabari waomba kuondolewa malipo usajili mitandao ya kijamii

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KLABU ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Dodoma (CPC), imeiomba serikali kuondoa malipo ya usajili wa mitandao ya kijamii inayomilikiwa na vilabu vya waandishi wa habari kwa kuwa haiendeshwi kibiashara bali inatoa huduma za kuhabarisha jamii.

Mwenyekiti wa CPC, Mussa Yusuph, alitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa akisoma risala ya klabu hiyo kwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Kundo Mathew, kwenye hafla ya usiku wa waandishi wa habari mkoani Dodoma iliyoandaliwa na CPC kwa udhamini wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Taasisi ya Wazo Huru.

Alisema kwa niaba ya vilabu 28 vya waandishi wa habari nchini wanaomba serikali kutoa msamaha wa malipo hayo na kwamba mara kadhaa wameshindwa kulipia Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA).

Aidha, aliwaomba wadau kusaidia kutatua kero zinazoikabili klabu hiyo ikiwamo uhaba wa vitendea kazi na ujenzi wa ofisi ili kubeba idadi kubwa ya wanachama.

"Ofisi yetu kwa sasa imekuwa ndogo hivyo kushindwa kukidhi kubeba idadi kubwa ya wanachama kwa wakati mmoja, pia tuna tatizo kubwa la thamani za ofisi hivyo tunapata changamoto kubwa pindi waandishi wengi wanapohitaji kutumia ofisi kwa wakati mmoja."

"Uhaba wa vitendea kazi kwa wanachama hasa kipindi ambacho Mkoa unakuwa na shughuli nyingi na kubwa kama vikao vya Bunge na mikutano ya kitaifa, vifaa hivyo ni kamera na kompyuta,"alisema.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Naibu Waziri Kundo aliahidi kutembelea ofisi za klabu hiyo na kuangalia namna ya kusaidia kutatua changamoto zilizobainishwa.

Alisema: "Nipongeze Klabu ya Dodoma kwa hatua hii kubwa ya kuwa na blogu, nipongeze pia kwa kuwa na ofisi napenda niwahakikishie serikali itaendelea kuwa pamoja nanyi hasa ikizingatiwa serikali imehamia Dodoma, Wizara pamoja na wadau tutaendelea kutatua changamoto za sekta ya habari."

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameendelea kuboresha mazingira ya waandishi wa habari na kuweka misingi ya kisheria ili kupata taarifa.

Alisema: "Katika gharama ya usajili wa blogs, Rais aliagizwa zipitiwe upya na zikapitiwa na tutaendelea kufanya mapitio ili kufikia hatua ambayo kweli itasaidia wanahabari."



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, akikabidhiwa tuzo jana kwa kujali muda wakati wa utekelezaji wa majukumu na Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Tamasha la Usiku wa Habari Dodoma, Sakina Abdulmasoud, aliyotunukiwa Februari 17, wakati wa Tamasha la Usiku wa Habari lililoandaliwa na Klabu ya Waandishi wa Habari mkoani humo (CPC). Kulia ni Mwanachama wa CPC, Augusta Njoji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wataalamu wa mkojo Hospitali ya Mkapa kujengewa uwezo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HOSPITALI ya Benjamin Mkapa (BMH) imeingia makubaliano ya ushirikiano na Chuo Kikuu cha Tiba cha Vienna, Australia kwa ajili ya kuwajengea uwezo wataalamu wa mfumo wa mkojo hapa nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Alphonce Chandika, alisema makubaliano hayo yatawezesha wataalamu wa mfumo wa mkojo wa BMH kwenda Chuo Kikuu cha Tiba cha Vienna kuongeza ujuzi na kupunguza wagonjwa kwenda kutibiwa nje ya nchi.

"Makubaliano haya yatasaidia kupunguza rufani nje ya nchi kwa kuwezesha wataalamu wa Chuo Kikuu cha Tiba cha Vienna kuja Tanzania na kufanya kambi ya pamoja na wataalamu wetu," alisema Dk. Chandika.

Aidha, alisema kwenye makubaliano hayo watagharamia utafiti pamoja na ubunifu na kuweka kambi hiyo ili kuhakikisha wanafikia malengo waliokusudia.

Katika makubaliano hayo yaliyosainiwa na Dk. Chandika na Naibu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Tiba cha Vienna, Dk. Michaela Fritz, yameshuhudiwa na Kaimu Balozi wa Tanzania nchini Australia, Elizabeth Rwitunga.

Dk. Fritz alisema makubaliano hayo yatasaidia kuwajengea uwezo wataalamu wa mfumo wa mkojo wa BMH ili kuzidi kuimarisha kitengo hicho.

Alisema hatua hiyo itazidi kuimarisha uhusiano kati ya nchi hizi mbili katika upande wa masuala ya sekta ya afya na kuongeza kuwa makubaliano hayo yatazidi kuimarisha kitengo cha wataalamu wa mfumo wa mkojo hospitalini hapo.

Naibu Mkuu wa Chuo cha Tiba cha Vienna, Dk. Fritz, alipongeza Tanzania kutokana na kuwekeza kwenye sekta ya afya.

# BAKWATA yatoa onyo kwa mashehe wazembe

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Wilaya ya Dodoma limewaonya mashehe wa wilaya na kata wataoshindwa kufanya kazi kwa weledi, kwamba wataenguliwa kwenye nafasi zao.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Baraza hilo, Bashiru Hussen, aliyasema hayo wakati akizungumza na viongozi wa ngazi mbalimbali wakiwamo wanafunzi wa madrasa na waumini kwenye Msikiti wa Chang'ombe ulioko jijini Dodoma.

Alisema BAKWATA wilaya kamwe haitakuwa tayari kufanya kazi na viongozi wasioendana na kasi iliyoko ambao wamezoea kufanya shughuli zao za kidini na kijamii kwa mazoea.

"Bakwata wilaya inataka viongozi wake watakaofanya kazi zao kwa faida ya kuisaidia dini ya kiislamu pamoja na serikali kwa lengo la kuleta maendeleo ya kiuchumi kwa waumini,"alisema.

Hivyo aliwataka kujituma katika kazi zao kwa kujitambua wao wenyewe badala ya kusubiri kusimamiwa kwenye nafasi walizoaminiwa na baraza na waumini wenyewe.

"Mimi kama kiongozi wenu ninawaomba mjisimamie nyinyi wenyewe, badala ya kusubiri kusimamiwe. Fanyeni kazi kwa malengo ya BAKWATA huku mkijiepusha kufanya kazi kwa mazoea,"alisema.

Pia aliwahimiza viongozi hao kuwatumikia waumini wao pamoja na kuisaidia serikali katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo.

Wajumbe wa Baraza la Bakwata Mkoa akiwamo Shehe Said Rajabu na Shehe Abdulli Azizilal, wakizungumza na viongozi na waumini kwenye msikiti huo waliwataka watu kuachana na vitendo viovu vinavyosababisha kuwapo kwa ukatili hapa nchini.

Waliwataka wananchi wakijiepusha na vitendo viovu ili kudumisha amani yake tofauti na ilivyo kwa hivi sasa.



# Tanzania, Malawi zaunda kamisheni ya pamoja Bonde la Mto Songwe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TANZANIA na Malawi zimeunda kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe unaotenganisha nchi hizo ili kushirikiana kutatua matatizo yanayosababishwa na mto huo pamoja na kuendeleza rasilimali kwa maendeleo ya pande zote mbili.

Aidha, kila nchi imeunda jukwaa la wadau wa bonde la mto huo kwa ajili ya kujadiliana namna sahihi ya kuendeleza rasilimali zilizoko na kuangalia namna ya kuendeleza ushirikiano baina ya mataifa hayo jirani.

Akizindua jukwaa hilo na kufungua kikao cha kamisheni ya pamoja, Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, alisema mto huo ni muhimu kwa pande zote mbili kutokana na kuwa miongoni mwa mito michache inayotenganisha mataifa mawili.

Aliwataka wadau hao kuendeleza ushirikiano ili kuhakikisha pande zote zinanufaika na rasilimali za mto huo ikiwamo shughuli za kilimo, uvuvi na huduma zingine ambazo zinatarajiwa kuanzishwa kutokana na uwapo wa mto huo. Alisema bonde hilo lina ukubwa wa mraba 4,203 na linajumuisha wilaya saba za nchi zote mbili za Tanzania na Malawi na kwamba eneo hilo linahitaji usimamizi mkubwa.

Alizitaja wilaya zinazonufaika na bonde hilo kuwa ni Mbozi, Ileje na Wilaya ya Mbeya kwa upande wa Tanzania na kwa upande wa Malawi ni Wilaya ya Chitipa na Kalonga.

"Matarajio yetu ni kuanzisha mradi wa pamoja wa uzalishaji wa umeme kwa kujenga mabwawa ambayo pia yatatumika kwenye kilimo cha umwagiliaji na hata kupeleka maji kwa wananchi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani," alisema Mahundi.

Alisema Tanzania na Malawi ni mataifa marafiki ambayo yamekuwa yakishirikiana kwa muda mrefu na kwamba uendelezaji wa mto huo utasaidia kuimarisha ushirikiano wa kidiplomasia.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji kutoka Wizara ya Maji, Pamela Temu, alisema lengo la kikao hicho ilikuwa ni kubadilishana uzoefu baina ya wadau wa pande hizo mbili.

Alisema kikao hicho kililenga kuunganisha nguvu ya kifedha na kutafuta vyanzo vya mapato kwa ajili ya kuendeleza rasilimali za bonde la mto huo ikiwa ni pamoja na kuanzisha miradi ya maendeleo kwa ajili ya kuwanufaisha wananchi.

Temu alisema katika hatua ya awali ya uendelezaji wa rasilimali za mto huo wanakusudia kujenga bwawa kwa ajili ya kuzalisha umeme pamoja na ufugaji wa samaki.

Alisema awamu ya pili itahusisha ujenzi wa huduma za kijamii ikiwa ni pamoja na usambazaji wa maji kwa wananchi, ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya, ujenzi wa shule pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya barabara.

"Awamu ya tatu itahusisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwa ajili ya kilimo cha mazao mbalimbali mbalimbali ikiwamo mpunga, kwa sasa tunaunganisha nguvu ili tuwe na uwezo wa kuendeleza huduma hizi," alisema Temu.

Mkurugenzi wa Bonde la Ziwa Nyasa, Eunice Engbert, alisema Mto Songwe ni miongoni mwa mito nane mikubwa ambayo inamwaga maji ndani ya Ziwa Nyasa.

Alisema upo mto mmoja uitwao Shile ambao ndio unatoa maji ndani ya Ziwa Nyasa kupeleka katika Mto Zambezi na kwamba mto huo una umuhimu mkubwa kwa wananchi wa Malawi.

Hivyo, aliwataka wananchi wa pande zote mbili kuhakikisha wanatunza vyanzo vya maji ili kuhakikisha rasilimali za ziwa hilo zinakuwa endelevu na kusaidia maendeleo ya mataifa hayo mawili.



Vijana wa Itifaki wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya wakimvalisha skafu Mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, alipofanya ziara ya kujitambulisha juzi. Kulia ni Katibu wa Itikadi na Uenezi Mkoa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wanafunzi darasa la saba waliofeli kupelekwa vyuoni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATOTO zaidi ya 3,000 waliofeli mitihani ya darasa la saba mwaka jana mkoani Mbeya na kukosa sifa za kuendelea na masomo ya sekondari, wanatarajiwa kujiunga na vyuo mbalimbali vya ufundi mkoani humo ili wapate ujuzi utakaowasaidia kujiajiri.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maendeleo ya sekta ya elimu katika mkoa huo.

Alisema serikali ya mkoa huo imeanzisha utaratibu huo ili kuepusha ndoto za watoto hao kufa na wao kugeuka kuwa watoto wa mtaani na wasiokuwa na ajira zenye staha kutokana na kutokuwa na ujuzi wa aina yoyote.

Alisema vijana hao watajiunga na vyuo mbalimbali vikiwamo vya Ufundi Stadi (VETA), vyuo vya maendeleo ya jamii na wengine watajiunga na elimu ya watu wazima na kwamba kila mwanafunzi atachagua kile anachotaka kusomea.

Homera alisema lengo la serikali ni kuzalisha mafundi wengi ambao watasaidia kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika mkoa huo pamoja na kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana. Alisema mafunzo watakayokuwa wanayapata vijana hao yatakuwa yenye gharama nafuu kulingana na chuo ambacho mwanafunzi husika atachaguliwa kwenda kusoma.

Alisema mpaka sasa tayari watoto hao wamepangwa kwenye vyuo hivyo katika kila wilaya ya mkoa huo na wazazi wataendelea kuhamasishwa ili washirikiane na serikali kwenye uendeshaji wa mafunzo hayo.

# CCM yaiomba serikali kuwalipa fidia wakazi vijiji vitano

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, kimeomba serikali kuwalipa fidia baadhi ya wananchi waliondolewa kwenye vijiji vitano vilivyokuwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ili iwasaidie kwenda kuanzisha makazi mapya kwenye maeneo watakayohamia.

Aidha, kimeiomba serikali kuwatafutia wananchi hao mashamba na maeneo ya kufugia mbadala ili wakaendeleze shughuli zao za kilimo na ufugaji ambazo ndizo vyanzo vikuu vya uchumi wao.

Mjumbe wa Halmashauri Kuuu ya Wilaya ya Mbarali, Christopher Uhagile, alitoa ombi hilo juzi wakati wa ziara ya Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela.

Mwaselela anaendelea na ziara katika wilaya zote za Mkoa wa Mbeya kwa ajili ya kujitambulisha kwa wanachama baada ya kuchaguliwa na Halmashauri Kuu ya chama hicho Mkoa wa Mbeya. Uhagile aliipongeza serikali kwa kuamua kurekebisha mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa kubadili Tangazo la Serikali Namba 28 la Mwaka 2008 (GN.28) ambalo mipaka yake ilisababisha mgogoro baina ya wananchi na hifadhi hiyo.

Alisema mipaka ya hifadhi hiyo ilikuwa imechukua maeneo mengi ya wananchi na hivyo kuwafanya wawe wanashindwa kufanya shughuli zao za uzalishaji mali kwa amani wakihofia kuondolewa na serikali.

"Tunaishukuru sana serikali kwa kuifuta GN. 28 ambayo imetutesa wananchi wa Mbarali kwa zaidi ya miaka 15, sasa tunaomba serikali itusaidie pia kuwatafutia maeneo ya kulima wananchi wa vijiji vitano ambavyo vilibainika kuwa vipo kwenye eneo muhimu," alisema Uhagile.

Alisema awali vijiji 39 vilikuwa vipo ndani ya hifadhi na vilikuwa vinatakiwa kuondolewa lakini baada ya serikali kurekebisha mipaka hiyo ni vijiji vitano pekee ambavyo vinaondolewa jambo ambalo alisema limesaidia kuumaliza mgogoro.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbarali, Mary Mbwilo, alimpongeza Mwaselela kwa kushinda uchaguzi huku akimtaka kufanya kazi ya kukisaidia chama hicho na kuepuka kusikiliza majungu.

Alisema wakati wa uchaguzi huwa kunakuwa na mambo mengi ambayo wakati mwingine huwa yanawagawa wanachama lakini baada ya kukamilika kwa uchaguzi anayeshinda anakuwa na wajibu wa kuwaunganisha wanachama wote.

Mbwilo alisema wanachama wa chama hicho katika wilaya yake ni wamoja na wanafanya kazi kwa ushirikiano ili kuhakikisha wanaisaidia serikali kutimiza wajibu wake.

Akijitambulisha kwa wajumbe, Mwaselela alisema katika kipindi cha uongozi wake atahakikisha anawaunganisha wanachama wa chama hicho katika majimbo yote ili chama hicho kiendelee kushinda nafasi mbalimbali za uchaguzi.

Hivyo, aliwataka viongozi wa chama hicho na wajumbe wa halmashauri kuu kuhakikisha wanayasema mazuri yote ambayo chama hicho kimewafanyia wananchi ili kukiimarisha.

Pia aliwataka viongozi wa chama hicho kuepuka kusemana vibaya hadharani na badala yake watumie vikao halali vya chama kurekebishana kama kuna sehemu wanaona makosa.





# Rais Mwinyi: Teknolojia ya nyuklia imetokomeza mbung'o

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema mafanikio yaliyopatikana Zanzibar kutokana na matumizi ya teknolojia ya nyuklia ni kutokomeza wadudu aina ya mbung'o ambao wamekuwa wakiathiri afya na uzalishaji wa mifugo.

Alisema Tanzania imeingia mikataba na maridhiano mbalimbali ya kikanda na kimataifa juu ya udhibiti wa matumizi salama ya mionzi na teknolojia ya nyuklia.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki Dunga Wilaya ya Kati Unguja wakati akiweka jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi wa ofisi na maabara za tume ya nguvu za atomiki.

Dk. Mwinyi alisema kuwapo kwa maabara hizo kutaongeza ufanisi katika kusimamia usalama wa mionzi na kuimarisha afya za wananchi.

Alisema mradi huo utawezesha kuimarisha biashara na kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi.

"Tayari nchi yetu imefaidika kupitia mikataba na maridhiano hayo. Hivyo natumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki pamoja na washirika wingine wa maendeleo kwa misaada mbalimbali wanayotoa,"alisema.

Alisema miongoni mwa misaada hiyo ni kuimarisha miundombinu, vifaa na utaalamu unaohitajika katika utafiti, ubunifu, udhibiti na matumizi salama ya mionzi na teknolojia ya nyuklia. Alisema taifa linatumia teknolojia ya nyuklia katika nyanja mbalimbali, hivyo usimamizi na udhibiti wa matumizi salama ya vyanzo vya mionzi nchini ni jambo muhimu.

Dk. Mwinyi aliwataka wafanyakazi wa tume ya nguvu ya atomiki kufanyakazi kwa bidii ili wafanikishe mipango iliyopo pamoja na kubuni miradi zaidi kwa faida ya nchi.

Hata hivyo alisema sayansi na teknolojia ya nyuklia ina manufaa makubwa na hivyo ikitumika vizuri, itasaidia kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta mbalimbali za uchumi kama sekta za kilimo, mifugo, nishati, pamoja na afya.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui alisema wizara hiyo ni wadau wakubwa wa sekta ya atomiki kwa sababu wanamiradi mikubwa inayojengwa ambayo inatumia mionzi. Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Juma Kipanga, alisema watahakikisha ujenzi huo unakamilika kwa wakati na ubora unaotakiwa na kuwa katika viwango vya kimataifa.

Alipongeza Serikali ya Zanzibar kwa kutoa eneo la ujenzi na kugharamia ujenzi wa barabara katika eneo hilo ambalo limerahisisha ufikiaji wa miundombinu.

Mkurugenzi Mkuu wa TAEC, Profesa Lazaro Busagala, alisema ujenzi huo utagharimu shilingi bilioni tatu na utakapokamilika utakuwa na faida nyingi ikiwamo kuongeza tija katika utekelezaji wa sera ya taifa ya teknolojia ya nyuklia ya mwaka 2015.

Alisema pia mradi huo, utawezesha wafanyabiashara na wananchi kutekeleza mpango wa kurahisisha na kuendeleza biashara nchini na kukuza uchumi wa wananchi.



Mke wa Rais wa Zanzibar ambaye ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation, Mariam Mwinyi (mwenye nguo ya pinki), akiongoza matembezi ya kilometa tatu ya kupinga vitendo vya udhalilishaji kwa watoto jana. **PICHA: IKULU**

# Kamati yakoshwa ujenzi Uwanja wa Ndege Pemba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMATI ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar imesema mradi wa uimarishaji wa Uwanja wa Ndege wa Pemba ni miongoni mwa hatua za serikali za kuifungua Pemba kiuchumi. Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa kamati hiyo, Yahya Rashid Abdallah, wakati akiwasilisha ripoti ya kamati katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Chukwani.

Alisema utafiti wa kamati umebaini kwamba hatua za ujenzi zitaanza baada ya kukamilika hatua za ukusanyaji wa vifaa kwa mjenzi huyo na serikali kukamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yataathiriwa na ujenzi huo.

Alisema kutokuwekwa uzio eneo la kilomita moja lililobakia, kutokuwa na gari ya uhakika la zimamoto na uokoaji na ukosefu wa huduma za kibenki ni mojawapo ya changamoto zinazoukabili uwanja huo.

Aidha, alisema wizara husika ihakikishe inaongeza mashine za ukaguzi wa mizigo ikiwa ni hatua mojawapo ya kuimarisha usalama kiwanjani hapo.

Alisema pia wizara ihakikishe inaimarisha ofisi zote zilizoko katika Uwanja wa Ndege wa Pemba zitakazowezesha taasisi zote zinazotoa huduma kiwanjani hapo kufanya shughuli zao kwa ufanisi mzuri kulingana na wakati wa sasa ikiwamo mtandao wa intaneti na huduma za kibenki ili kufanikisha huduma zinazotolewa kiwanjani hapo kukidhi haja.

Akizungumzia kuhusu Bandari ya Malindi Unguja, alisema Wizara ya Miundombinu, Uchukuzi na Mawasiliano ihakikishe hatima njema kwa wafanyakazi wa Bandari ya Malindi wakati inaelekea katika kukabidhiwa kwa mwekezaji wa kuendesha bandari hiyo.

"Kamati inashauri wizara kupitia Bandari ya Malindi kuimarisha huduma katika maeneo yote hasa katika eneo la kushukia abiria ili kuondosha msongamano ulioko sasa,"alisema.

Alisema kamati inashauri kuliangalia kwa kina suala la uingiaji na utokaji wa magari ya mizigo kutoka nje ya zanzibar, kwani kumekuwa na malalamiko ya wadau kuhusiana na kutumika vibaya magari hayo na kuikoseha serikali mapato.

# Ataka kampuni vileo zinazojihusisha na magendo kufutwa

**Na Mwandishi Wetu**

MWANAHARAKATI wa Haki za Binadamu na Utawala Bora, Ali Makame Issa, amesema kampuni za vileo zinazojihusisha na biashara za magendo zinapaswa kufutwa ili kulinda upotevu wa mapato ya serikali.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu sakata la Kampuni ya MGW 2014 Enterprises kutuhumiwa kuingiza vileo vya magendo na kuhifadhiwa katika ghala la kampuni hiyo lililoko Amani Mkoa wa Mjini Magharib Unguja.

"Biashara ya magendo inasababisha hasara kubwa ya mapato kwa serikali hasa magendo ya vileo kutokana na thamani yake, mamlaka za ukusanyaji kodi lazima zichukue hatua kudhibiti mianya hiyo,"alisema Makame.

Alisema kampuni zilizopewa kibali cha kuingiza pombe Zanzibar ni kampuni tatu ambazo ni Scoch, One Stop Center na ZMMI ambazo ndizo zilizoshinda zabuni kwa mujibu wa Sheria ya Vileo ya Mwaka 2020.

Hata hivyo alisema pamoja na kampuni hizo kuruhusiwa kisheria, lakini Jeshi la Wananchi JWTZ nao wamekuwa wakiingiza vileo jambo ambalo halileti sura nzuri katika kusimamia sheria hiyo.

Alisema kwamba lengo la kutungwa sheria hiyo ililenga kuziba mianya ya ukwepaji wa kodi kupitia biashara ya vileo pamoja na uingizaji holela wa pombe Zanzibar.

Hata hivyo iliipongeza Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), kwa kuahidi kuchunguza sakata hilo, muda mfupi baada ya kujitokeza.

Aidha alisema inasikitisha kuona Bodi ya Vileo imelegeza masharti kwa kushindwa kusimamia sheria ipasavyo jambo ambalo linatia wasiwasi wa kuwapo kwa mianya ya rushwa ndio maana sheria ya vileo inashindwa kusimamiwa ipasavyo.

Hata hivyo alimpongeza Rais wa Zanzibar kwa hatua anazoendelea kuchukua za kupambana na ubadhirifu wa mali za umma.

Alisema misingi ya utawala bora inaonekana kuimarika Zanzibar, kutokana na kuongezeka kwa uwajibikaji kwa watumishi wa umma na serikali kufanikiwa kudhibiti vitendo vya ubadhirifu wa mali za umma pamoja na mafisadi kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Akizungumzia suala hilo msimamizi wa Kampuni ya MGW 2014 Enterprises, Ali Seif, alikanusha kampuni yake kuhusishwa na biashara ya magendo.

# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI**
**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Shauri la Madai Ndoa Na. 247/2022**
**Jina la mdai: DIAMOND TRUST BANK TANZANIA LTD**
**Jina la Mdaiwa: JACOB MUSSA MAGINA ILLULAH**

### KUITWA SHAURINI MDAIWA
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: JACOB MUSSA MAGINA ILLULAH**
Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba
**FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA KUJIBU SHITAKA LINALO KUKABILI**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 8 Mwezi wa 3 Mwaka 2023 saa 3:00 asubuhi/Mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 15 Mwezi wa 2 Mwaka 2023.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KINONDONI
WILAYA YA KINONDONI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI**
**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Shauri la Madai Ndoa Na. 250/2022**
**Jina la mdai: DIAMOND TRUST BANK TANZANIA LTD**
**Jina la Mdaiwa: JACOB MUSSA MAGINA ILLULAH**
**PATRICK RUTTA KAJWA HURA**

### KUITWA SHAURINI MDAIWA
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: PATRICK RUTTA KAJWA HURA**
Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba
**FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA KUJIBU MASHITAKA YANAYO KUKABILI**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 8 Mwezi wa 3 Mwaka 2023 saa 3:00 asubuhi/Mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 15 Mwezi wa 2 Mwaka 2023.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KINONDONI
WILAYA YA KINONDONI

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ATHUMANI RASHIDI HAGWE** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina **UPENDO YESAYA NDOSSI** aina ya **BOXER** namba za usajili **MC 751 CHB.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/678998/2023**

---

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRIC T DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 11 OF 2023**

**In Matter of the Estate of the Late LAZARO KITUNDU LAZARO**
**By 1. GEORGE LAZARO KITUNDU**
**2. ..................................**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grand should be field on or before the **07** day of **3 / 2023.**
Dated at **Morogoro**, this **07** day of **02, 2022**

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**MAHAKAMA YA WILAYA DODOMA**
**CIVIL APPEAL 1/2023**
**Shauri la Rufaa Jinai/Madai Na. 1/2023**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya MAKOLE PC**
**JAMES I. MSECHU..................MRUFANI**
**DHIDI YA**
**LUCAS LUCAS.........................MRUFANIWA**

**KWA: LUCAS LUCAS**
Kwa rufaa iliyotajwa hapo juu itasikilizwa katika mahakama iliyotajwa hapo juu siku ya IJUMAA tarehe 10/3 /2023. Unatakiwa uhudhurie katika mahakama hiyo Mrufani/Mrufaniwa/Shahidi pamoja na vielelezo vyovyote kama vipo.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na mhuri wa mahakama hii leo tarehe 9 mwezi 02 mwaka 2023

MAHAKAMA YA WILAYA DODOMA

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LUDOVICK S.L. UTOUH** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba **T 709 ALU** Mitsubishi Pajero Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu au awasiliane na Ludovick S.L. Utouh kwa simu namba **0787 981045** au **0713320425.**
**POLISI TAARIFA: DAR/KM/RB/60262/2023**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**
**CIVIL CASE 19/2022**
**MWAJABU SELEMAN SALOZI. ............APPLICANT/ PLANTIFF**
**VERSUS**
- **MOHAMED SELEMAN MINTANGA**
- **SAID SALIM SAID**
- **ZANZIBAR INSURANCE CORPORATION.........RESPONDENT**

**TO:**
- **MOHAMED SELEMAN MINTANGA**
- **SAID SALIM SAID**
- **ZANZIBAR INSURANCE CORPORATION**

### NOTICE OF DATE OF MENTION/HEARING
**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for hearing/mention on 28 day of 02, 2023 at 9:00 am
Before Hon N.J. TUNGARAJA RM/SRM
YOUR ARE required to appear in this court on the fixed date without fail and you may bring with you all required documents in support of your case.
Given under my hand and the seal of the court this 15 day of February,2023

RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRICT
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**RAPHAEL F JEREMIAH NALIJA** Anatangaza kupotelewa kwa Vyeti vya chuo kilichotolewa na chuo kikuu cha **ST.AUGUSTINE (MOROGORO)**. Cheti cha level ya certificate (saint Augustine) chenye Reg **No.BAF/0012/2019** pamoja na Trancript.Kwa yeyote atakaeiona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi au piga simu namba **0717857441, DSM/PHQ/RB/68191/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI**
**Mkoa DAR-ES-SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi Na. 234/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU KASHINDI TUNU MIGEZO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA REHEMA YOHANA KIMAZI**

### TANGAZO
**(Kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 27 Mwezi 02 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 13 Mwezi 02 Mwaka 2023

HAKIMU

---

*OFISI ZA MATANGAZO*
*Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.*
*Mobile: +255 - 745 700 710.*
*E-mail: advertise@guardian.co.tz,*
*Website: www.ippmedia.com*

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

The Guardian
The Home of Great Newspaper
Our Regional Offices and Representatives




*Feel free to contact for:*
ADVERTISEMENT ON NEWSPAPERS / DIGITAL PLATFORMS
AND SUBSCRIBING NEWSPAPERS / E-PAPERS

HEAD OFFICE
THE GUARDIAN LIMITED
MIKOCHENI AREA
P.o.Box 31042, Dar es salaam, Tanzania
Tel: + 255 745700710 | Email: info@guardian.co.tz

Nipashe @Nipashetz
The Guardian @Theguardiantz
IPPmedia

---

Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Sky Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O.Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania
Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

## TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA WA WATANZANIA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | AINA NA SEHEMU YA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SADA ABDALLAH LAISER | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - TEGETA WAZO | KISAONI GENERAL AUCTION TANZANIA LIMITED | 08-03-2023 |
| 2 | ANANIA GUREN MNKENI | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - MALAMBA MAWILI | KISAONI GENERAL AUCTION TANZANIA LIMITED | 08-03-2023 |
| 3 | NASHON MARWA NYAMUHANGA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - BUZA MAKANGARAWE | DIAMOND CREDIT RECOVERY COMPANY LIMITED | 08-03-2023 |
| 4 | NATHANAEL KINYONYI T/A NASSA ITELEMI KINYONYI | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - KIBAHA PWANI | WHITE MIRACLES (T) LTD | 08-03-2023 |
| 5 | PATRICK JULIUS KENDAMVANO | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - KIBAMBA | JOFORTE AUCTION MART COMPANY | 08-03-2023 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika ofisi za wakuu wa wilaya wanaohusika.

**MASHARTI YA MNADA;**
- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# AU kuanzisha mchakato maridhiano Libya

**ADDIS ABABA,** ETHIOPIA

UMOJA wa Afrika (AU) umesema unaratibu mkutano wa maridhiano ya kitaifa kwa ajili ya Libya, ikiwa ni jaribio la mwisho la kurejesha hali ya utulivu katika taifa hilo lililoharibiwa na vita.

Tamko hilo limetolewa katika siku ya mwisho ya mkutano wa kilele wa umoja huo uliofanyika makao yake makuu, mjini Addis Ababa nchini Ethiopia.

Mwenyekiti wa Halmashauri Kuu ya Umoja wa Afrika, Moussa Faki Mahamat, aliliambia shirika la habari la AFP, kwamba, wamefanikiwa kukutana na pande tofauti tofauti na sasa wapo katika mchakato wa kushirikiana nao kuhusiana na maandalizi ya siku na mahali patakapofanyika mkutano huo.

Mahamat alisema, mkutano huo utaongozwa na mpatanishi mkuu wa umoja huo nchini Libya, ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Kongo, Denis Sassou Nguesso.

Libya imejikuta katika mzozo tangu mwaka 2011, baada ya kuangushwa kwa utawala wa Moamer Kadhafi, katika uasi unaodaiwa kuungwa mkono na wanajeshi wa jumuiya ya kujihami ya NATO.

Tangu mwezi Machi mwaka jana, serikali ya Libya ya upande wa mashariki inayoongozwa na mbabe wa kivita Khalifa Haftar, mwenye mahusiano ya karibu na Russia na Misri imekuwa ikiishutumu serikali inayotambuliwa na Umoja wa Mataifa, inayoongozwa na waziri mkuu Abdullamid Dbeibah, ikidai imepitisha muda wake mamlakani.

Mapema mwezi huu, Umoja wa Mataifa ulitangaza kwamba maofisa waandamizi kutoka serikali hizo zinazokinzana wameanzisha utaratibu wa kuwaondoa wanajeshi wa kigeni pamoja na mamluki.

Hata hivyo, mjadala ulioongozwa na mjumbe wa umoja huo, Abdoulaye Bathily, ulishindwa kuandaa ratiba ama hatua madhubuti za kuondolewa kwa wanajeshi hao, waliotarajiwa kufikia 20,000 mwaka 2021, kulingana na Umoja huo.

Mbali na Libya, Umoja huo pia umezungumzia sera yake ya kutokuvumilia kabisa mabadiliko yasiyo ya kikatiba, huku ikisema itaendelea kuyasimamisha mataifa yanayoongozwa na tawala za kijeshi.

Aidha, inaelezwa kuwa mataifa ya ukanda wa Sahel ya Burkina Faso, Guinea na Mali na Sudan yalisimamishwa uanachama kwenye umoja huo kutokana na mapinduzi ya miaka ya karibuni, ingawa, kamishna wa mahusiano ya siasa, amani na usalama wa umoja huo Bankole Adeoye, aliashiria utayari wa kuyasaidia kurejea kwenye utawala wa kidemokrasia.

"Halmashauri iko tayari kuyasaidia mataifa wanachama kurejea kwenye utaratibu wa kikatiba. Cha muhimu ni kwamba demokrasia inatakiwa kuchukua mkondo wake, inatakiwa kupiganiwa na kulindwa," alisema Adeoye.

Naye Rais wa Kenya, William Ruto, alitoa wito kwa mataifa tajiri kuwajibishwa kwa kuchochea ongezeko la joto ulimwenguni na mabadiliko kwenye taasisi za kifedha za kimataifa kama miongoni mwa hatua za kukabiliana vema na mabadiliko ya tabianchi, suala ambalo pia lilitawala katika mkutano huo.

Pia alisisitiza kwamba mataifa maskini na hususan ya Afrika yamekumbwa na athari kubwa za mabadiliko hayo na kuchochea ukame na mafuriko licha ya kuchangia kidogo kwenye uzalishaji wa gesi ukaa.

**DW**



Mkuu wa Jeshi la Burkina Faso, Kanali Adam Nere, akipokea bendera kwa Luteni Kanali wa Jeshi la Ufaransa, Louis Lecacheur, wakati wa makabidhiano kuashiria kuondoka kwa vikosi vya Ufaransa katika kambi ya Kamboincin juzi. Picha: **VOA**

# Ufaransa yaondoka rasmi Burkina Faso

**OUAGADOUGOU,** BURKINA FASO

JESHI la Burkina Faso limesema limesimamisha rasmi operesheni za kijeshi kati ya nchi hiyo na jeshi la Ufaransa katika taifa hilo la Afrika Magharibi.

Januari mwaka huu, Burkina Faso iliipa Ufaransa mwezi mmoja kuondoa vikosi vyake wakati ikimaliza makubaliano ya kijeshi, yaliyoruhusu vikosi vya Ufaransa kupambana na waasi katika himaya yake, ikielezea kuwa nchi itajilinda yenyewe.

Inaelezwa kuwa kuondoka kwao kunafungua ukurasa mpya kwa Burkina Faso kukabiliana na makundi ya kiislamu yenye uhusiano na Al Qaida na Islamic State, ambayo yamechukua eneo kubwa la ardhi na kusababisha maelfu ya watu kukosa makazi katika eneo pana la Sahel, kusini mwa Jangwa la Sahara. Mkuu wa vikosi vya Jeshi la Burkina Faso, alisema jeshi lao limeshiriki chini ya uongozi wa vikosi maalumu vya Ufaransa, Sabre, katika kushusha bendera na kuadhimisha rasmi kumalizika kwa kikosi kazi cha operesheni katika ardhi ya Burkina Faso.

Wizara inayohusika na mambo ya kijeshi ya Ufaransa haikujibu lolote ilipoulizwa kutoa maoni yake.

Kuondoka kwa takriban wanajeshi 400 wa kikosi maalumu cha Ufaransa, nchini Burkina Faso kunafuatia kudorora kwa uhusiano ambao umejumuisha kwa Ouagadougou kuitaka Ufaransa kumwondoa balozi wake.

Mwaka jana maadamano ya kupinga uwepo wa Jeshi la Ufaransa, yaliongezeka maradufu kutokana na mtazamo kwamba Ufaransa haikufanya lolote katika kukabiliana na wanamgambo.

Katika wiki zilizopita, makundi madogo ya waandamanaji wanaopinga uwepo wa Ufaransa, yamekuwa yakikutana kila jioni mjini Ouagadougou kuangalia kama kuna dalili za Ufaransa kuondoka. **VOA**

## Jamii yasisitizwa kuepuka ubaguzi nchini DRC

**KINSHASA,** DRC

GAVANA wa Jimbo la Kivu Kaskazini, nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Luteni Kanali Constant Ndima, ametoa wito kwa wananchi katika eneo hilo kuacha vitendo vya ubaguzi na badala yake kuvumilia kipindi cha uchaguzi kiendeshwe kwa utulivu.

Gavana huyo alitoa wito huo jana baada ya kuzuka madai na hofu kuwa watu wasio raia wa taifa hilo wanajiandikisha.

Wananchi nchini DRC wakati huu wanaendelea na zoezi la kijiandikisha kwa ajili ya kupiga kura katika uchaguzi mkuu utaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwaka huu nchini humo.

Naye msemaji wa jimbo la Kivu Luteni Kanali Njike Kaiko, kudhalilishwa kwa jamii yoyote katika eneo hilo.

"Kwa kuzingatia mvutano ambao jimbo la Kivu Kaskazini linapitia kuhusu vita vya M23 na ADF, Gavana Constant Ndima ametoa wito kwa raia wote kujiepusha na vitendo vya kudhalilishwa jamii yoyote ile," alisisitiza Kaiko.

Tume ya Uchaguzi ilianza zoezi la kuwasajili wapigakura katika majimbo ya Mashariki mwa nchi hiyo wiki iliyopita, kuelekea uchaguzi wa mwezi Desemba. **RFI**

## Biden afanya ziara ya kushtukiza Ukraine

**KYIV,** UKRAINE

RAIS wa Marekani, Joe Biden, amewasili mjini Kyiv kwa kushtukiza ikiwa ni ziara yake ya kwanza nchini Ukraine tangu Russia ilipovamia takribani mwaka mmoja uliopita.

Ziara hiyo ya kushtukiza imekuja wakati alipokuwa akisafiri kwenda nchi jirani ya Poland kukutana na Rais Andrzej Duda.

Dakika chache Rais wa Ukraine Zelensky, alishirikisha picha kwenye akaunti yake rasmi ya Telegram akipeana mkono na Rais wa Marekani.

Pia inaelezwa kuwa kulikuwa na uvumi mapema jana kwamba mgeni muhimu alikuwa akiwasili katika mji mkuu wa Ukraine, huku mwanasiasa wa Ukraine Lesia Vasylenko akithibitisha kuwa ni Rais Biden. **BBC**

# KILI MARATHON YATANGAZA BARABARA ZITAKAZOFUNGWA

**Na Mwandishi Wetu**

ZIKIWA zimebakia siku chache kabla ya kufanyika mbio maarufu za Kilimanjaro Premium Lager International Marathon kwa mwaka huu, waandaaji wa mbio hizo wametoa maelezo na maelekezo kuhusu kufungwa kwa baadhi ya barabara na shughuli zingine kadhaa na hivyo kubadili mwenendo wa baadhi za shughuli katika Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro Jumapili wiki hii.

Kwa mujibu wa waandaaji hao, maelekezo hayo yanalenga kuwasaidia wakazi wa Moshi na wale wa maeneo ya jirani kupanga safari zao mapema na kutumia njia mbadala pale inapohitajika ili kutoa nafasi kwa mbio hizo kufanyika kwa usalama kama inavyotarajiwa.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Barabara ya Sokoine kutoka kona ya KCMC hadi Barabara ya Kilimanjaro, zitafungwa kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa 3:30 asubuhi, ambapo wenye magari wanashauriwa kutumia njia mbadala za kwenda katikati ya mji wa Moshi kupitia eneo la Shanty Town na Kata ya Rau hadi eneo la Mweka lililoko Kibosho.

**Pia, Barabara ya Kilimanjaro hadi kona ya Barabara ya Sokoine inayoelekea Hospitali ya Rufani ya KCMC itafungwa kuanzia saa 1:45 asubuhi hadi saa 3:30 asubuhi.**

"Hatua hii itatoa fursa kwa washirki wanaofika eneo la kuanzia mbio hizi kupata maeneo ya maegesho katika viwanja vya Shule ya Polisi Tanzania (CCP), pamoja na eneo la lango Kuu la Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) lililoko barabara ya kuelekea Uru sambamba na kupata nafasi ya kutosha kwa washiriki wakati wa kuanza kwa mbio hizo", ilieleza taarifa hiyo.

Taarifa hiyo pia ilieleza Barabara ya Masoka hadi Mweka kupitia eneo la Kibosho pia kuanzia saa 12:30 asubuhi hadi saa 2:30 asubuhi itafungwa.

Aidha, ilieleza hakutakuwa na maegesho katika Barabara ya Sokoine kutokea kona ya Barabara ya Kilimanjaro ambao taarifa hiyo imeonya kwamba gari lolote litakaloegeshwa eneo hilo litachukuliwa na maofisa wa polisi wa kikosi cha usalama barabarani.

"Kutakuwa na maegesho ya bure kwenye eneo la Shule ya Polisi (CCP), ambapo wanaotaka kuegesha vyombo vyao vya moto wataingilia kupitia Barabara ya Kilimanjaro na eneo ambalo mbio za Nusu Marathon za Tigo (Tigo Half Marathon) zitaanzia.

"Pia, kutakuwa na maegesho ya bure kwenye eneo lenye kivuli kizuri katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) ambalo linaweza kufikiwa kwa kupitia barabara inayoelekea Uru tu; eneo hilo ni mwendo wa dakika tano tu kutoka uwanjani hadi eneo ambalo mbio za kilomita tano na zile za kilomita 21 zitaanzia na dakika mbili kutoka pale za kilomita 42 zitakapoanzia.

"Jeshi la Polisi kupitia kikosi chake cha usalama barabarani linatarajiwa kudhibiti masuala yote ya barabarani katika barabara zote kuanzia muda wa saa 12 asubuhi hadi saa 6:30 mchana, ambapo madereva wameshauriwa kuwa waangalifu na makini ili kuhakikisha usalama wa washiriki wa mbio hizo", ilisema taarifa ya hiyo ya wandaaji.

Wakati huo huo, zoezi la ukusanyaji wa namba na vifaa kwa ajili ya ushiriki wa mbio hizo mwaka huu, unatarajiwa kufanyika jijini Arusha leo na kesho, kuanzia saa nane mchana hadi saa 11 jioni katika Hoteli ya Kibo Palace.

Wadhamini wa mwaka huu ni pamoja na wadhamini wakuu Kilimanjaro Premium Lager (Km. 42), Km. 21 za Tigo (Tigo Half Marathon), kilomita tano za kujifurahisha chini ya udhamini wa Grand Malt, wadhamini wa meza za maji TPC Sugar, Simba Cement, Kilimanjaro Water, TotalEnergies, wanaoungwa mkono na wadhamini wengine ambao ni pamoja na Kibo Palace Hotel, CMC Automobiles, KK Security and Keys Hotel.

## Singida BS na nafasi ya tatu

**Na Hadija Mngwai**

SINGIDA Big Stars imeamua kufukuza mwizi kimya kimya kutokana na kupiga hesabu kali katika michezo yake saba iliyobakia ya Ligi Kuu Bara huku ikiwaombea mabaya wapinzani wao, Azam FC kupoteza mechi zake ili kuweza kumaliza nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara.

Singida ambayo ipo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 44 ikicheza mechi 23, moja mbele ya Azam FC yenye pointi 43, imejipanga kumaliza Ligi Kuu Bara ikiwa katika nafasi tatu za juu kwa kuwaombea wapinzani wao hao kupoteza ili kujihakikishia nafasi hiyo.

Kwa sasa Singida Big Star imebakisha michezo saba dhidi ya Mtibwa Sugar mechi itakayochezwa Februari 27, Polisi Tanzania Aprili 14 yote ikipigwa Uwanja wa Liti Singida, Coastal Union (Mkwakwani) Machi 12 huku mchezo dhidi ya KMC ukitarajiwa kuchezwa Uwanja wa Uhuru.

Aidha, michezo ya Yanga na Ruvu Shooting ambayo haijapangwa tarehe bado pia itapigwa Uwanja wa Liti kabla ya kutupa karata yake ya mwisho ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Namungo Mei 28, mwaka huu katika Uwanja wa Majaliwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Singida Big Star, Hussein Masanza, alisema wamejipanga kikamilifu katika ratiba yao hiyo ili kuweza kupata pointi tatu katika kila mchezo na kutimiza malengo ya kumaliza nafasi tatu za juu kwa kuamini wapinzani wao watapoteza.

"Tumefurahi kuona tupo nafasi ya tatu ya msimamo wa Ligi Kuu Bara kwa kuwapita pointi moja Azam naamini wanaweza kupoteza, lengo letu ni kuona tunaendeleza ushindi katika michezo yetu saba iliyobakia ili kumaliza katika nafasi tatu za juu.

"Tunahitaji kutumia vema uwanja wetu wa nyumbani katika michezo yetu minne ili kupata alama 12 zitakazotuweka katika nafasi nzuri ya kufikia malengo yetu ya kumaliza katika nafasi za juu," alisema Masanza.

**WANGU HUU...**



Mchezaji wa Timu ya Bulls, Aqram Issa (katikati), akimiliki mpira dhidi ya beki wa timu ya Bhoki Youth Academy, wakati wa mazoezi ya kujiandaa na mashindano ya Dar Youth Cup kwenye viwanja vya Mikocheni jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# *Polisi Zanzibar yapania kubaki Ligi Kuu*

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

LICHA ya kuwa na msimu mbaya wa Ligi Kuu Zanzibar, Kocha Msaidizi wa timu ya Polisi, Yusuph Sape, amesema "tutahakikisha hatushuki daraja".

Polisi FC ipo nafasi ya 13 ikiwa na alama 19 katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya kushuka dimbani mara 21, ikishinda michezo minne, sare saba na kupoteza mechi 10.

Akizungumza na gazeti hili jana, Sape alisema japo bado wapo katika mstari mwekundu wa kushuka daraja, lakini watahakikisha michezo iliyobaki wanafanya vizuri ili kuibakisha timu hiyo katika Ligi Kuu.

Alisema wanahitaji jitihada zaidi ili kuhakikisha wanafanikiwa kuibakisha timu hiyo Ligi kuu ambapo wanamatumaini makubwa kwa kuwa timu zilizo juu yao zinatofautiana alama chache.

Alisema licha ya kubaki michezo michache ya kukamilisha msimu, kumekuwapo na ushindani mkubwa kwa timu ambazo zipo katika mbio za ubingwa na zile zinazohitaji kubaki Ligi Kuu.

"Tumesogea baada ya ushindi wa mchezo wetu wa 21, tupo nafasi ambayo tukishinda michezo mitatu basi tutakuwa sehemu salama, hata hivyo tusielekeze katika michezo mitatu maana timu sita kuja chini kunatofauti ya alama chache sana, hivyo kila timu inapiga mahesabu yake," alisema Sape.

Hata hivyo, Sape alisema katika mchezo wa 22 dhidi ya Maafande wa JKU, utakuwa mgumu na wa ushindani kwa kuwa wapinzani wao malengo yao makubwa ni kuwa katika timu nne za juu wakati huu kiwa nafasi ya tano.

Ligi Kuu Zanzibar mzunguko wa 22 utaendelea keshokutwa, Alhamisi ambapo Mlandege FC watawakaribisha Jamhuri SC katika Uwanja wa Amaan majira ya saa 10 alasiri.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ZIYECH AWINDWA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich imeungana na Paris St-Germain katika mbio za kumsajili winga wa Chelsea na Morocco, Hakim Ziyech, 29. (***Fijaches***)

### GVARDIOL AITAKA EPL

MLINZI wa kati wa RB Leipzig na Croatia, Josko Gvardiol, mwenye umri wa miaka 21, amesema anataka kucheza Ligi ya England (EPL), na alikuwa karibu kujiunga na Leeds United mwaka 2020 na karibia angesajiliwa na Chelsea msimu uliopita wa majira ya joto. (***Times***)

### POTTER HAFUKUZWI CHELSEA

MMLIKI wa Chelsea, Todd Boehly, hana nia ya kumfuta kazi kocha Graham Potter licha ya kufungwa kwa 'Blues' hao bao 1-0 na Southampton Jumamosi. (***Mirror***)

### RODRI AFUATILIWA BARCA

BARCELONA wanamfuatilia kwa karibu kiungo wa kati wa Manchester City na Hispania, Rodri, kabla ya dirisha la majira ya joto na watakuwa tayari kutoa pauni milioni 80 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. (***Football Insider***)

### SPURS YAMTAKA POCHETTINO

KLABU ya Tottenham Hotspur inamtaka kocha wao wa zamani, Mauricio Pochettino, kama mbadala wa Antonio Conte ikiwa Muitaliano huyo ataondoka Spurs mwishoni mwa msimu huu. (***Nicolo Schira***)

### NEWCASTLE KWA TIERNEY

KLABU ya Newcastle United inamfuatilia kwa karibu beki wa Arsenal na Scotland, Kieran Tierney, 25. (***Football Insider***)

### GLAZER KUSAIDIA FEDHA

FAMILIA ya Glazer imepewa usaidizi wa kifedha wa kusalia kama wamiliki wa Manchester United na uongozi wa Hedge Fund wa Marekani, Elliott baada ya kikundi hicho chenye makao yake makuu jijini New York kusajili nia ya kuwekeza katika klabu hiyo. (***ESPN***)

### THURAM KUTUA INTER

INTER Milan ndio walio mstari wa mbele kumsajili mshambuliaji wa Borussia Monchengladbach na Ufaransa, Marcus Thuram, mwenye umri wa miaka 25, mbele ya Manchester United na Bayern Munich. (***Calciomercato***)

### FERGUSON ANYATIWA SPURS

CHELSEA na Tottenham Hotspur zinafikiria kumnunua mshambuliaji wa Brighton wa Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson, 18. (***Sun***)

### GOMEZ ATAKIWA SEVILLA

KLABU ya Sevilla ina nia ya kupata mkataba wa mkopo kwa beki wa pembeni wa Manchester City, Sergio Gomez, 22. (***Fijaches***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# NEYMAR MAJANGA PSG

**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR hakuvunjika kifundo cha mguu katika ushindi wa Paris Saint-Germain dhidi ya Lille, lakini atalazimika kusubiri matokeo ya uchunguzi zaidi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, alitolewa nje kwa machela mapema katika kipindi cha pili pale Parc des Princes Jumapili baada ya kupata jeraha kwenye kifundo cha mguu wake wa kulia.

PSG walipata ushindi wa mabao 4-3 kutokana na mkwaju wa faulo wa dakika za lala salama wa Lionel Messi, lakini jeraha la Neymar linaleta wasiwasi, hasa wakitarajia mechi ya mkondo wa pili wa hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich Machi

**●●● Mwathiriwa wa kifundo cha mguu wakati wa mechi dhidi ya Lille, atafanyiwa tathmini mpya baada ya saa...**

8, mwaka huu.

**Kocha Christophe Galtier awali alihisi Neymar, ali yetengeneza bao la kuongoza la Kylian Mbappe na kufunga la pili la PSG, aliku wa ameteguka kifundo cha mguu na sasa imethibitishwa kuwa siyo.**

Hata hivyo, uchunguzi zaidi utahitajika ili kubaini kama kuna matatizo na mishipa.

"Mwathiriwa wa kifundo cha mguu wakati wa mechi dhidi ya Lille, Neymar alifanyiwa uchunguzi wa MRI Jumapili," ilisomeka taarifa ya PSG.

"Hii haikuonyesha kuvunjika. Tathmini mpya itafanywa baada ya saa 48."

Nuno Mendes pia alitolewa nje akiwa amejeruhiwa dhidi ya Lille, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno akionekana kuumia goti la kulia.

Kama Neymar, beki huyo wa pembeni atafanyiwa vipimo zaidi siku zijazo ili kuthibitisha ukubwa wa jereha lake.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,080,3

JACKPOT
MECHI WIKI HII

TAREHE: 21,22 NA 24 FEBRUARI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 21/02/23 | 22:45 | Rotherham vs Sunderland | 3.12 | 3.32 | 2.18 |
| 02. 21/02/23 | 22:45 | Swansea vs Stoke City | 2.20 | 3.22 | 3.17 |
| 03. 21/02/23 | 22:45 | Millwall vs Burnley | 2.88 | 3.22 | 2.37 |
| 04. 21/02/23 | 23:00 | Liverpool vs Real Madrid | 2.29 | 3.47 | 2.82 |
| 05. 22/02/23 | 02:05 | Tlaxcala FC vs CD Tapatio | 2.37 | 3.20 | 2.74 |
| 06. 23/02/23 | 17:00 | Bengaluru FC vs FC Goa | 2.39 | 3.47 | 2.54 |
| 07. 23/02/23 | 20:45 | SC Dnipro 1 vs AEK Larnaca | 2.22 | 3.30 | 3.15 |
| 08. 23/02/23 | 20:45 | PSV Eindhoven vs Sevilla FC | 2.21 | 3.50 | 3.00 |
| 09. 23/02/23 | 20:45 | Monaco vs Bayer Leverkusen | 2.22 | 3.50 | 3.00 |
| 10. 23/02/23 | 23:00 | FC Basel vs Trabzonspor | 2.30 | 3.39 | 2.94 |
| 11. 23/02/23 | 23:00 | Union Berlin vs Ajax | 2.25 | 3.19 | 3.19 |
| 12. 23/02/23 | 23:00 | Manchester Utd vs Barcelona | 2.38 | 3.26 | 2.92 |
| 13. 24/02/23 | 19:00 | HNK Sibenik vs Istra | 2.90 | 2.90 | 2.44 |

MSHINDI WA SUPA JACKPOT YA MECHI - 13




SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TEN HAG: MAN UNITED BADO INA KAZI KUBWA



**MANCHESTER,** England

KOCHA Erik ten Hag aliutaja uchezaji wa Manchester United katika kipindi cha kwanza kuwa "uchafu" licha ya kuwafunga Leicester City mabao 3-0 katika Uwanja wa Old Trafford, Jumapili.

United walitawala kipindi cha pili na kukwea hadi nafasi ya tatu kwenye msimamo wakipitwa pointi tano na vinara, Arsenal walio kileleni, lakini baadaye Ten Hag hakuficha kusikitishwa kwake na dakika 45 za kwanza.

"Kwa kweli sikufurahishwa na uchezaji wetu," alisema Ten Hag akiwaambia waandishi wa habari baada ya mechi.

"Lazima tufuate kanuni za uchezaji wetu, tusipofanya hivyo ni upuuzi. Tunapokutana na mpinzani mzuri kama Leicester tunatakiwa kupambana sana na bahati kwamba David De Gea alikuwa bora.

"Tulikuwa na bahati sana wakati wa kipindi cha kwanza kwamba tulikuwa bao moja mbele. Lilikuwa goli kubwa, lakini uchezaji wetu ulikuwa wa ovyo."


Ushindi dhidi ya Leicester ulikuja saa 48 baada ya ofa ya kwanza ya kununuliwa kwa klabu hiyo kuthibitishwa na mfanyabiashara wa benki kutoka Qatar, Sheikh Jassim Bin Hamad Al Thani na bilionea wa England, Sir Jim Ratcliffe.

United wana mechi ya Ligi ya Europa dhidi ya Barcelona na fainali ya Kombe la Carabao dhidi ya Newcastle Jumapili na Ten Hag amewaambia wachezaji wake kwamba hawawezi wanatakiwa kuwa makini.

"Tumejitolea kwa klabu hii," alisema kocha huyo.

"Ni klabu yetu na ipo mioyoni mwetu, tunapaswa kuzingatia uchezaji wetu na kufanya vizuri na hivyo ndivyo wachezaji na wafanyakazi wanapaswa kufanya."

# Thuram anukia Chelsea, Inter



**MUNICH,** Ujerumani

MARCUS Thuram yuko tayari kuondoka Borussia Monchengladbach kwa uhamisho wa bila malipo mwishoni mwa msimu huu huku kukiwa na taarifa za kuwaniwa kutakiwa Chelsea na Inter Milan.

Mkurugenzi wa Michezo wa Gladbach, Roland Virkus, alitoa dalili ya wazi zaidi siku ya Jumapili kwamba Gladbach itashindwa kumbakiza mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa Juni.

Klabu nyingi za Ulaya zimetajwa kuhitaji kumnunua Thuram, huku Inter ikiripotiwa kuwa inaongoza katika mbio pamoja na Chelsea na wapinzani wa Gladbach wa Bundesliga, Bayern Munich.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, amefunga mabao 11 na kusaidia mengine matatu kwenye Bundesliga msimu huu.

Virkus, akizungumza na Sport1, alionekana kukiri uwezekano wa kushindwa katika majaribio ya Gladbach ya kumbakisha mtoto huyo wa gwiji wa Ufaransa, Lilian Thuram.

Alisema: "Tukiwa na Marcus Thuram, lakini sidhani kama tunaweza kumbakiza. Inabidi tukubali hilo wakati kuna klabu kubwa zaidi ambako Marcus anaweza kwenda."

Virkus aliongeza: "Ukweli kwamba wachezaji watatuacha bure si hali nzuri na siwezi kuizuia."

Gladbach inashikilia nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, baada ya Thuram kufunga katika ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya wachezaji 10 wa Bayern Jumamosi.

# 318,061/-

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/02/23 | 18:00 | Everton FC vs Aston Villa | 2.60 | 3.15 | 2.75 |
| 02. 25/02/23 | 18:00 | Birmingham City vs Luton Town | 2.90 | 3.15 | 2.45 |
| 03. 25/02/23 | 18:00 | Bristol City vs Hull City | 2.31 | 3.25 | 3.05 |
| 04. 25/02/23 | 18:00 | Queens Park Rangers vs Blackburn Rovers | 2.45 | 3.25 | 2.85 |
| 05. 25/02/23 | 18:00 | Stoke City vs Millwall FC | 2.49 | 3.15 | 2.85 |
| 06. 25/02/23 | 18:00 | West Bromwich Albion vs Middlesbrough FC | 2.46 | 3.20 | 2.85 |
| 07. 25/02/23 | 18:15 | Cadiz CF vs Rayo Vallecano | 2.85 | 3.10 | 2.55 |
| 08. 25/02/23 | 20:30 | Schalke 04 vs VfB Stuttgart | 3.00 | 3.30 | 2.31 |
| 09. 25/02/23 | 21:00 | Maritimo Madeira vs Santa Clara Azores | 2.50 | 3.10 | 2.85 |
| 10. 25/02/23 | 22:45 | US Lecce vs Sassuolo Calcio | 2.41 | 3.20 | 2.95 |
| 11. 25/02/23 | 23:00 | Valencia CF vs Real Sociedad San Sebastian | 2.85 | 3.20 | 2.48 |
| 12. 26/02/23 | 16:30 | Tottenham Hotspur vs Chelsea FC | 2.34 | 3.25 | 3.00 |
| 13. 26/02/23 | 17:00 | FC Nantes vs Stade Rennes | 3.20 | 3.20 | 2.23 |
| 14. 26/02/23 | 17:00 | Clermont Foot 63 vs Strasbourg Alsace | 2.28 | 3.20 | 3.15 |
| 15. 26/02/23 | 17:30 | SC Freiburg vs Bayer Leverkusen | 2.37 | 3.40 | 2.85 |
| 16. 26/02/23 | 18:30 | Rio Ave FC vs GD Chaves | 2.55 | 3.15 | 2.80 |
| 17. 26/02/23 | 18:30 | FC Lugano vs FC Basel 1893 | 2.45 | 3.25 | 2.36 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 21/02/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 5562 | PS Tni vs Psis Semarang | 2.53 | 3.06 | 2.65 |
| 15:45 | 4277 | Aswan vs Al Ahly Cairo | 8.16 | 4.58 | 1.36 |
| 15:55 | 3211 | AL Qaisoma vs Alshoulla | 2.48 | 2.75 | 3.01 |
| 16:30 | 4236 | Platinum City Rovers vs Casric Stars FC | 2.82 | 2.71 | 2.66 |
| 16:30 | 5666 | Uthongathi vs Baroka FC | 2.54 | 2.76 | 2.91 |
| 16:45 | 1275 | Qatar SC vs Al-Sailiya SC | 1.91 | 3.36 | 3.57 |
| 17:00 | 4210 | Rapide Oued Zem vs Athletic Youssoufia | 2.05 | 3.01 | 3.58 |
| 17:00 | 5684 | Luka Koper vs NK Radomlje | 1.57 | 3.95 | 4.78 |
| 18:00 | 4758 | Ismaily SC vs Ghazl EL Mahallah | 2.03 | 2.98 | 4.07 |
| 18:10 | 3438 | AL Nasr vs Al Jahra | 2.52 | 3.32 | 2.49 |
| 18:30 | 2010 | Qalali vs Malkiya Club | 3.25 | 3.15 | 1.93 |
| 18:30 | 2594 | Al Ittifaq Bhr vs Bouri | 1.96 | 3.15 | 3.15 |
| 18:30 | 2926 | Denguele Sport vs Stade Abidjan | 2.28 | 2.85 | 3.21 |
| 18:30 | 4155 | Um Alhassam vs AL Ittihad Bhr | 2.71 | 3.07 | 2.47 |
| 19:30 | 4537 | NK Mura vs Tabor Sezana | 1.64 | 3.78 | 4.45 |
| 20:00 | 4651 | Haras EL Hodood vs Farco FC | 2.88 | 2.58 | 2.93 |
| 20:15 | 2115 | Ittihad Tanger vs Maghreb Tetouan | 2.55 | 2.75 | 2.90 |
| 20:15 | 4584 | Germany W vs Sweden W | 1.67 | 3.48 | 4.67 |
| 22:30 | 1439 | Mouloudia Oujda vs Sccm Chabab Mohammedia | 2.52 | 2.79 | 2.89 |
| 22:45 | 1742 | Morecambe vs Port Vale | 3.12 | 3.27 | 2.20 |
| 22:45 | 1926 | Maidstone vs Eastleigh | 2.74 | 3.27 | 2.41 |
| 22:45 | 1944 | Woking vs Bromley | 1.72 | 3.61 | 4.39 |
| 22:45 | 2069 | Barnet vs Altrincham | 2.11 | 3.47 | 3.10 |
| 22:45 | 2264 | Rotherham vs Sunderland | 3.18 | 3.32 | 2.15 |
| 22:45 | 2820 | Dorking Wanderers vs Torquay | 2.39 | 3.52 | 2.61 |
| 22:45 | 2840 | York City vs Boreham Wood | 3.10 | 3.26 | 2.20 |
| 22:45 | 2918 | Wrexham vs Scunthorpe | 1.20 | 6.10 | 11.56 |
| 22:45 | 3017 | Gateshead vs Oldham | 2.32 | 3.41 | 2.78 |
| 22:45 | 3124 | Hamilton vs Inverness | 2.64 | 3.27 | 2.50 |
| 22:45 | 3646 | Chesterfield vs Wealdstone | 1.55 | 4.00 | 5.27 |
| 22:45 | 3940 | Fleetwood Town vs Cambridge Utd | 2.04 | 3.37 | 3.42 |
| 22:45 | 4121 | Notts County vs Southend | 1.50 | 4.14 | 5.66 |
| 22:45 | 4193 | Dagenham and Redbridge vs Aldershot | 2.06 | 3.36 | 3.31 |
| 22:45 | 4411 | Swansea vs Stoke City | 2.20 | 3.22 | 3.17 |
| 22:45 | 4463 | Maidenhead U vs Yeovil | 2.26 | 3.19 | 3.04 |
| 22:45 | 4484 | Ballymena Utd vs Larne | 7.24 | 4.35 | 1.37 |
| 22:45 | 4535 | Norwich City vs Birmingham | 1.62 | 3.81 | 4.95 |
| 22:45 | 4557 | Southport vs Spennymoor Town | 2.15 | 3.32 | 3.01 |
| 22:45 | 4570 | Welling vs Braintree | 2.21 | 3.46 | 2.79 |
| 22:45 | 4672 | Hartlepool vs Newport | 3.25 | 3.25 | 2.15 |
| 22:45 | 4679 | Millwall vs Burnley | 2.88 | 3.22 | 2.37 |
| 22:45 | 4886 | St.Albans vs Ebbsfleet | 3.32 | 3.43 | 1.97 |
| 22:45 | 5194 | Rochdale vs Stockport | 4.45 | 3.56 | 1.74 |
| 22:45 | 5332 | Albion Rovers vs Elgin City | 2.05 | 3.42 | 3.11 |
| 22:45 | 5468 | Walsall vs Crewe | 1.81 | 3.42 | 4.27 |
| 22:45 | 5498 | Blackburn vs Blackpool | 1.92 | 3.46 | 3.71 |
| 22:45 | 5609 | Halifax vs Solihull Moors | 2.57 | 3.31 | 2.54 |
| 23:00 | 2399 | Plymouth vs Cheltenham | 1.54 | 3.93 | 5.07 |
| 23:00 | 2738 | Liverpool vs Real Madrid | 2.26 | 3.46 | 2.87 |
| 23:00 | 2810 | Eintracht Frankfurt vs Napoli | 3.22 | 3.47 | 2.08 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MUDATHIR AFUNGUKA KUISAIDIA YANGA KICHAPO TP MAZEMBE

**Na Hadija Mngwai**

BAADA ya juzi kuwa miongoni mwa waliofanikisha ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya TP Mazembe kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika, Kiungo wa Yanga, Mudathir Yahaya, amesema amejisikia faraja kuifungia timu yake hiyo kwa kuwa walitoka kupoteza mchezo uliopita.

Yanga juzi ilitoka kifua mbele dhidi ya TP Mazembe ya DR Congo, kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, ikiwa ni wiki moja tangu ipoteze mchezo wake wa kwanza wa hatua hiyo ya makundi, ikiwa ugenini dhidi ya US Monastir ya Tunisia.

Mabao ya Yanga katika mchezo huo yalifungwa na mshambuliaji Mzambia Kennedy Musonda dakika ya saba, Mudathir Yahya dakika ya 11 na winga Mkongomani Tuisila Kisinda dakika za nyongeza huku bao pekee la Mazembe likifungwa na Alex Ngonga dakika ya 80.

Kwa matokeo hayo, Yanga sasa inashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Kundi D la Kombe la Shirikisho barani Afrika ambalo kinara ni US Monastir ikiwa na alama nne, TP Mazembe nafasi ya tatu kwa pointi zao tatu, huku Real Bamako ikiburuza mkia baada ya kuambulia alama moja tu katika michezo miwili ambayo kila timu imecheza.

Akizungumza na mwandishi wetu jana, kwanza kabisa Mudhathir alimshukuru Mungu kwa timu yake kuweza kupata alama tatu dhidi ya TP Mazembe, ambazo zimewasaidia kuwa katika nafasi nzuri.

"Ndio nimerudi uwanjani, nimejisikia faraja kubwa kupata pointi tatu hizi nyumbani kwa sababu tumeshapoteza mchezo uliopita, pointi hizi zitatusaidia, tumekuja tumejipanga, tunamshukuru Mungu alhamdulilah kwa hilo," alisema Mudathir.

Katika mchezo mwingine wa Kundi D uliochezwa juzi, ulizikutanisha timu za Real Bamako na US Monastir ambapo matokeo yalikuwa sare ya bao 1-1.

Yanga itashuka tena dimbani Jumapili wiki hii ambapo itakuwa ugenini nchini Mali dhidi ya vibonde wa kundi hilo, Real Bamako, wakati TP Mazembe ikiwakaribisha US Monastir jijini, Lubumbashi.

**HUNIWEZI...**



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, akimiliki mpira kwa kifua dhidi ya mchezaji wa TP Mazembe kwenye mechi ya hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na kumalizika kwa wenyeji kushinda mabao 3-1. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Nabi ataja sababu 3 kuiua Mazembe*

INATOKA UK 24

kuzembea," alisema.

Kwa ushindi huo, Yanga imekabidhiwa zawadi ya Sh. milioni 33 ikiwa ni Sh. milioni 15 kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ambaye aliahidi kununua kila bao kwa Sh. milioni tano, huku zingine zikitoka kwa wadau mbalimbali wa soka nchini.

Akikabidhi fedha hizo kutoka kwa rais baada ya mechi hiyo juzi, Msemaji wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema anakabidhi fedha hizo kutoka kwa rais na kwamba anataka kuona wachezaji wakipigania ushindi katika kila mechi.

"Ninakabidhi Sh. milioni 15 kutoka kwa rais, ambaye alihidi Sh. milioni tano kwa kila goli, bahati nzuri wadau wengine nao wamechangia akiwamo Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wiraza ya Michezo na DRFA (Chama cha Soka Mkoa wa Dar es Salaam), hivyo jumla nakabidhi Sh. milioni 33," alisema Msigwa.

Kwa upande wa wachezaji wa Yanga, wakiongozwa na nahodha wao, Bakari Mwamnyeto, ambaye alipokea kitita hicho kutoka kwa Makamu wa Rais wa klabu hiyo, Arafat Ally, walieleza furaha yao huku wakitaka fedha hizo wagawane pale pale kila mtu aondoke na chake.

Jesus Moloko alikuwa akiimba "makuta eeee", akiwa na maana kwa lugha ya Kilingala, pesa, huku Farid Mussa akimpa ushauri Mwamnyeto pesa hizo wagawane muda huo huo.

"Mama aliahidi na sisi tumeweza kukamilisha ahadi yake ya kushinda mabao 3-1, basi na yeye ametekeleza ametupa Sh. milioni 15. Kuhusu mechi ilikuwa ngumu sana, baada ya mechi hii sasa tunataka kila mechi kupata pointi tatu ili kwenda kwenye hatua inayofuata. "Nawataka wanachama na mashabiki wa Yanga waje kwa wingi zaidi ya hivi kwenye mechi zinazofuata na sisi tutawapa mambo mazuri, sisi ndiyo jeshi lao, au vipi straika wangu?" Alisema na baadaye kumuuliza Fiston Mayele ambaye naye alitoa ya kwake.

Mayele alisema ana furaha kubwa kuifunga TP Mazembe kwa sababu ilikuwa ni kama mechi ya 'dabi' ya DR Congo iliyochezwa nchini Tanzania.

Michezo

Nipashe Jumanne Februari 21, 2023



Neymar majanga PSG UKURASA 21

# Nabi ataja sababu 3 kuiua Mazembe

●●● Wapewa milioni 33 kutoka kwa Rais Samia na wadau wa soka, mzuka wa ushindi sasa...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ametaja mambo matatu yaliyokifanya kikosi chake kuibuka na ushindi wa mabao 3 -1 juzi dhidi ya TP Mazembe kwenye mechi ya hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika huku akianza kwa kusema "hasira ya kupoteza nchini Tunisia".

Yanga ilifanikiwa kuibuka na ushindi huo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi, baada ya kutoka kuchezea kichapo ugenini cha mabao 2-0 dhidi ya US Monastir ya Tunisia katika mchezo wao wa awali wa hatua ya makundi.

Akizungumzia na gazeti hili, Nabi alisema haina maana amefika mwisho wa ubora wa timu yake na kwamba anaendelea kukinoa kikosi chake kuwa bora zaidi hasa katika michuano ya kimataifa.

Alisema anawapongeza wachezaji wake kwa kucheza vizuri na wamejituma tofauti na walivyocheza mechi iliyopita dhidi ya US Monastir ya Tunisia huku akitaja sababu tatu zilizowafanya kuibuka na ushindi kuwa ni wachezaji wake kupambana katika kila dakika kuanzia ya kwanza hadi 90 na kutumia vizuri nafasi wanazotengeneza na kupata bao la mapema ambalo liliwavuruga wapinzani.

Lakini alisema sababu kubwa ya Yanga kupata matokeo, ni maneno ya watu kuwatia hasira baada ya kupoteza Tunisia.

"Huu ushindi hauna maana ndio umefika mwisho, ile asilimia 100 bado haijafikia na bado nitaendelea kutengeneza timu kwa sababu nimeona mapungufu katika mchezo wetu wa leo (juzi), tukitoka hapa tunaenda kufanyia kazi," alisema Nabi

Kocha Msaidizi wa TP Mazembe, Pamphile Mihayo Kazembe, alisema kipindi cha kwanza hawakucheza vizuri na Yanga kutumia udhaifu wao kwa kupata bao la mapema.

Alisema bao la kwanza na la pili liliwavuruga, lakini kipindi cha pili walifanikiwa kubadilika na kupata bao la kwanza ambalo liliwarejesha mchezoni.

"Tulifanya makosa mengine na kuruhusu bao la tatu na kupotea kabisa, tumejifunza kikosi tulichoanza nacho hakikucheza tulivyotarajia na

INAENDELEA UK 23




Winga wa Yanga, Jesus Moloko, akikokota mpira baada ya kumtoka mchezaji wa TP Mazembe kwenye mechi ya hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na kumalizika kwa wenyeji kushinda mabao 3-1. **Na Mpigapicha Wetu**

## Simba hasira CAF kwa Azam FC leo

**Na Saada Akida**

BAADA ya Wawakilishi wa Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba kukamilisha mechi ya pili ya michuano hiyo ya kimataifa bila ushindi, hasira zao za kupoteza leo wanazielekeza katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC.

Jumamosi Simba ilipoteza mechi ya kwanza ya nyumbani ya kimataifa kwa kufungwa mabao 3-0 na Raja Casablanca katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na leo wanashuka katika dimba hilo kuikaribisha Azam FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara.

Katika mchezo wa leo, Simba wataingia na hasira mara mbili ikiwa na kumbukumbu ya kupoteza alama muhimu katika mchezo wa kimataifa Jumamosi, lakini kuhitaji kulipa kisasi baada ya kufungwa bao 1-0 na Azam FC, katika mchezo wa duru la kwanza, bao pekee likifungwa na Prince Dube.

Timu zote mbili zikihitaji matokeo katika mchezo wa leo ambapo Simba wakiendelea na mbio zao ubingwa na kutaka kuwashusha Yanga ambao wako kileleni kwa pointi 59 huku Azam FC wakiwa nafasi ya nne kwa pointi 43 nyuma ya Singida Big Stars yenye alama 44.

Azam FC itawakosa wachezaji wawili muhimu wakitumikia adhabu ya kadi za njano ambao ni Idrissa Mbombo na Bruce Kangwa, Simba watashuka wakiwa na kikosi kamili huku Jonas Mkude akitarajiwa kupata nafasi ya kucheza katika mchezo huo. Kuelekea mchezo huo Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliviera, alisema baada ya kupoteza mechi ya kimataifa wamerudi uwanja wa mazoezi na tayari kwa ajili ya kutafuta pointi tatu dhidi ya Azam FC.

"Tunasahau matokeo ya mechi iliyopita na sasa akili na nguvu zetu kwa tunarejea uwanjani, kwa sababu ya kupoteza mechi mbili haina maana kwamba hatuna wachezaji wazuri," alisema Robertinho.

Alisema licha ya kutafuta pointi katika mchezo wa leo dhidi ya Azam FC pia anatumia mchezo huo kwa ajili ya maandalizi ya mechi ijayo dhidi ya Vipers ya Uganda.

Kocha huyo alisema anaimani kikosi chake kipo vizuri hususan safu ya ushambuliaji ambayo yuko Kibu Denis, Jean Baleke na Mosses Phiri kwa ajili ya kuwapa matokeo mazuri dhidi ya Azam FC na itawapa Morali kuelekea mechi ya kimataifa.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, John Matambala, alisema wamejiandaa vizuri dhidi ya Simba kwa kwenda kutafuta pointi tatu muhimu.

"Tumejipanga vizuri tunatambua Simba wataingia kivingine kwa sababu wametoka kupata matokeo mabaya katika michuano ya kimataifa, tutacheza kwa tahadhari kubwa kikubwa tunahitqji pointi tatu," alisema Matambala.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >